RESTORATION CHURCH OF CHRIST MINISTRIES

SONGBOOK

BARUT CONGREGATION
P. O. BOX 10250
NAKURU, KENYA

1. UMOJA

1. Mungu baba na Yesu Kristo
   wako na umoja. Uwezo hupatikana
   kwao ndio wenye mapenzi

   Kweli: Rehema na neema na Amani
   zitakuwa pamoja nasi. x2

2. Salamianeni wote wandugu
   na wadada na wamama
   Tusalamianeni Wakristo.
   katika jina Ia Kristo.

3. Paulo na Barnaba walipo
   rudi kule Antiokia.
   Waliwaeleza Wakristo
   Aliyoyafanya Mungu.

4. Mungu ameshatuunganisha
   na Wakristo wenzetu.
   Kwa kuihubiri injili
   na Kusaiamiana.

2. JINA LA YESU

1. Jina la Yesu liinuliwe
   (Jina la Yesu linaokoa) x2
   Jina la nguvu zote

2. Jina Ia Yesu Iinaokoa
   (Jina la Yesu lipewe sifa) x2
   Jina la nguvu zote

3. Jina Ia Yesu lina uwezo
   (Jina la Yesu lina uwezo) x2
   Jina la nguvu zote.

4. Jina la Yesu libarikiwe
   (Jina Ia Yesu libarikiwe) x2
   Jina Ia nguvu zote.

3. UPENDO

(I Wakorintho 13:1-13)

1. Nijaposema kwa lugha
   Kushinda malaika jameni,
   kama mimi sina upendo
   mimi ni kitu bure.

   Upendo hauna wive
   Upendo hauoni Mabaya
   Upendo huvumilia
   Upendo haujivuni.

2. Nijapohubiri sana
   kushinda unabii jameni
   kama mimi sina upendo
   Mimi ni kitu bure.

3. Nijapotoa mali yangu
   Kuwapa maskini jameni,
   Kama mimi sina upendo
   Mimi ni kitu bure.

4. Nijapokuwa na imani
   kuhamisha milima jameni
   kama mimi sina upendo.
   mimi ni kitu bure.

4. BWANA AMENITUMA

1. Bwana amenituma niende nikahubiri x2
   Kwa wandugu nikahubiri, kwa wadada nikahubiri

2. Bwana amenituma niende nikahubiri x2
   Kwa watoto nikahubiri kwa wa mama nikahubiri

3, Bwana amenituma niende nikahubiri x2
   Kwa wachawi kwa walevi nikahubiri

4. Bwana amenituma niende nikahubiri x2
   Popote nikahubiri Bwana amenituma niende nikahubiri

5. SIKU ZA MWISHO

1. Siku za mwisho ni nyakati hizi
   Wenye imani wamewekwa
   kati imani yao ijaribiwe
   Bwana naomba unisaidie x2

   Vumilia roho yangu, Majaribu ni kama moto
   lnayochoma imani yangu, Bwana naomba unisaidie x2

2. Naja kwako Bwana shetani hapana
   Ndani yangu niwe salama
   Unifiche nisionekane
   Bwana naomba unisaidie x2

3. Roho yangu usiogope
   Kuja kwake Roho wa kweli
   Jitakaze mbali na dhambi
   Bwana naomba unisaidie x2

4. Ukilemewa na majaribu
   Usimkubali mwovu shetani
   Mfukuze kwa jina la Yesu
   Bwana naomba unisaidie x2

6. KATIKA MJI WA TARSO

1. Katika mji wa Tarso
   Mji wake vikia
   Palikuwa kijana mmoja
   Jina lake Sauli

   Sauli, Sauli, Kijana wa Tarso
   Alikuwa mtezi, kaomba barua
   Kuwatesa wakristo x2

2. Sauli alitesa watu
   Wanaume na wake
   Kuwapeleka gerezani
   Huko Yerusalemu

3. Alipokuwa akienda
   Walifika njiani
   Akaanguka kifudifudi
   Na sauti ikatoka

   Ni mimi x2 ni Bwana, Unayenitesa leo
   — Halleluya , Simama uende mjini
   Ukapate wokovu x2

7. NAMDHANIA YESU MWOKOZI

1. Namdhania Yesu mwokozi
   nafanya dhambi ninazopenda x2

   Wanahubiri - watu wa Mungu
   Lakini mimi nimejitenga
   Najidanganya na ulimwengu
   Ambao kesho nitaucha.

2. Shetani naye anakasana
   Sababu yake muda mfupi. x2

3. Wandugu zangu mnaonaje
   Hii dunia na raha zake. x2

4. Muda kidogo tutaonana
   Kule mbinguni mbele ya Mungu x2

8. YESU NDIYE MZABIBU

1. Mimi ndimi mzabibu wa kweli
   Na Baba yangu ndiye mkulima
   Mimi ndimi mzabibu wa kweli
   Na Baba yangu ndiye mkulima.

   Tawi ndani yangu lisilozaa
   Nitaliondoa na kulitupa x2

2. Tawi Iizaalo matunda mema
   Husafishwa ili kuzaa mengi
   Tawi lizaalo matunda mema
   Husafishwa ili kuzaa mengi

3. Ninyi mumesafishwa kuwa safi
   Kwa kuwa ninyi mko ndani yangu
   Ninyi mmesafishwa kuwa safi
   Kwa kuwa ninyi mko ndani yangu.

9. SHANGILIA

1. Bwana alikufa, kwa ajili yangu
   ili tuokolewe, to-ka dhambini
   Mshukuruni Bwana, Kwa kuwa ni mwema
   Kwa maana fa-dhili zake ni za milele

   (oh..) Shangilia
   (ah..) Shangilia
   (ah..) Shangilia Yesu akupenda x2

2. Nami nafurahi, Yesu kaniokoa
   Tutakuwa naye, hu-ko mbinguni
   Nawe ndugu yangu, u-jiulize
   Utakuwa wapi, a-takaporudi x2

10. SAFARI YA KUNGOJA

1. Safari ya kungoja mtu wa Mungu
   Ya kwenda mbinguni ilipo ahidiwa
   Sisi tuwasafiri asema Bwana
   Safari ya tungoja

   Nawe utakwenda mbinguni
   Wokovu ndiyo njia yako
   Nawe utakwenda mbinguni
   Ndiyo makao yako

2. Niujumbe kwako wee mtu Mungu
   Yesu akuita aliye tufia
   Ujiunge nasi katika safari

3. Hapa duniani kuna shida nyingi
   Tamaa za mwili na ugumu wa maisha
   Njoo kwake Yesu ili akuokoe

11. YESU ALIKUFA

1. Bwana alikufa, kwa ajili yangu
   Ili tuokolewe, to-ka dhambini
   Mshukuruni Bwana, kwa kuwa ni mwema
   Kwa fa-dhili zake ni za milele x2

   (oh..) Shangilia
   (ah..) Shangilia
   (ah..) Shangilia Yesu atupenda x2

2. Nami nafurahi, Yesu kaniokoa
   Tutakuwa naye hu-ko mbinguni
   Nawe ndugu yangu u-jiulize
   Utakuwa wapi, a-takaporudi x2

12. PELELEZA NDANI YANGU

1. Peleleza ndani yangu, iwe safe nia,
   Kwangu kama kwako Mungu, idhihiri pia
2. Peleleza moyo wangu, unifunulie
   Yaliyomo ndani yangu, nami niyajue.
3. Kwanza osha dhambi zako, kumefunga giza
   Nijue ambavyo dhambi, niza kuchukiza.
4. Peleleza na mawazo, ni mbegu za mambo
   Asili ya machukizo, maumbuo-umbo.
5. Zidi kuyapeleleza, katikati yangu,
   hata mwisho, nifundishe udhaifu wangu.
6. Hapo nikikwinamia mbele yako Mungu,
   Hakika nitakujua, U mpenzi wangu.

13. TARUMBETA YAKE BWANA

1. Tarumbeta yake Bwana italia
   Na wale waliokufa wafufuke
   Tutakaribishwa na malaika mbinguni
   Na huko tutamuona mwana kondoo

   Asifiwe ni wapekee mwana kondoo
   Asifiwe ni mwana kondoo
   Asifiwe ni wa pekee mwana kondoo
   Na huko tutamuona mwana kondoo

2. Shida zetu duniani zitakwisha
   Tarumbeta yake Bwana ikilia
   Tutakwenda kumlaki Bwana Yesu
   Na huko tutamuona mwana kondoo

14. TAZAMA KULE KALVARI

1. Tazameni kule kalvari
   Mwokozi aliteswa na dhambi
   Alizikwa kule kaburini
   Mwishowe akatoka kwa ushindi.

   Nitashinda (Kweli) Nitashinda
   kama wewe pia ulishinda
   Nitapita mapitoni mwako
   Oh nimeanza Bwana nitashinda x2

2. Njia mbovu zote nimeacha
   Nitapita njia nyembamba
   Walipita Elia na Musa
   Walianza Bwana wakashinda

3. Kupokea nyimbo za ushindi
   Ulilnuliwa kwa mawingu
   Malaika kutwa wanaimba
   Wanasifu Nyimbo za ushindi.

15. MUNGU MTUKUFU ALIYE BWANA

1. Mungu mtukufu aliye Bwana
   Akamtoa Yesu mpendwa mwana
   Akawa dhabihu kwa dhambi zote,
   Kufungua njia kwa watu wote

   Msifuni, msifuni, Nchi imsikie;
   Msifuni, msifuni, Bwana Mshangilie
   Njooni kwake Baba, Kwa Yesu Mwana,
   Mpeni heshima, Aliye Bwana

2. Ukombozi wetu, tendo la Mungu
   Ni ukamilifu kwa kila mtu;
   Mwenye ukosefu akimwamini
   Atasamehewa na Yesu, kweli

3. Ametufundisha mambo ya mbingu
   Tukafurahishwa na Mwana Mungu
   Ametuinua tukae naye
   Atatuongoza hata milele.

16. MWANANGU KARIBU

1 Nilipopotea katika dhambini
Nilikuwa kama mwana mpotevu
Yesu alikuja kuniponya mimi
Akanirudisha kwa Babangu.

Mwanangu karibu, Mwanangu karibu
Tukae na Yesu Mwokozi wangu
Aliyeniponya kutoka dhambini
Akanirudisha kwa Babangu. x2

2. Malaika pale wananingojea
   Mji wa Kanaani wako na Yesu
   Aliyeniponya kutoka dhambi
   Akanirudisha kwa Babangu.

3. Nikienda mbinguni nitafurahia
   Nikae na Yesu Mwokozi wangu
   Aliyeniponya kutoka dhambini
   Akanirudisha kwa Babangu.

17. ANISIKIAYE ALIYE YOTE

1. Anisikiaye aliye yote;
   Sana litangae, wajue wote
   Duniani kote neno wapate,
   Atakaye na aje!

   Ni "Atakaye" ni "Atakaye"
   Pwani hata bara, na litangae;
   Ni Baba Mpenzi alinganaye
   Atakaye na aje.

2. Anijiliaye, Yesu asema,
   Asikawe, aje hima mapema;
   Ndimi njia, kweli, ndimi uzima:
   Atakaye na aje!

3. Atakaye aje, ndiyo ahadi;
   Atakaye hiyo, haitarudi!
   Atakaye lake, ni la ahadi!
   Atakaye na aje.

18. TUNAOMBA ROHO

1. Sauti yako ee Bwana
   Twaisikia utwitapo x2

   Tunaomba Roho Mtakatifu
   Ndiye aje atuongoze Bwana
   Tunajua tuwakosaji sisi
   Ewe Bwana utuokoe x2

2. Zikikoma siku zetu
   Utatwita juu mbinguni x2

3. Duniani tu wageni
   Tumo safarini wote x2

4. Tunaomba sana Bwana
   Siku hiyo tukaribishe x2

5. Mungu Baba Mungu mwana i
   Mungu Roho Mtakatifu x2

19. OMBI

1. Mungu wetu mwaminifu
   Ametuahidi sisi
   Kusikia na kujibu
   Kama tukiomba kwake.

   (Mungu) Mungu atatusikia, (Kama) Kama tukiomba kwake
   (Twende) Twende sasa na imani, (Kweti) Kweli atatusikia

2. Mungu atatupa sisi
   Vitu vyote kututosha
   Kitu gani ni kizuri
   Tutakipokea kwake.

3. Tusiogope kumwambia
   Mahitaji yetu yote
   Au makubwa au madogo
   Anapenda kusikia

4. Kwa furaha au huzuni
   Kila nchi na saa zote
   Tunaweza kumwombea
   Naye atatusikia.

20. SIONI HAYA KWA BWANA

1. Sioni haya kwa Bwana
   Kwake nitang'ara, mti wake sitakana
   Ni neno imara

   Msalaba ndio asili ya mema
   Nitatua mzigo hapo
   Nina uzima, furaha daima
   Njooni kafurahini papo

2. Kama kiti chake vivyo
   Ni yake ahadi, alivyowekewa navyo
   Kamwe havirudi.

3. Bwana Wangu, tena Mungu
   Ndilo lake jina. Hataacha roho yangu
   Wala kunikana

4. Atakiri langu jina
   Mbele za Babaye; Anipe pahali tena
   Mbinguni nikae

21. NIMEKUBALI KUMFUATA YESU

1. Nimekubali kumfuata Yesu
   Nimekubali kumfuata Yesu
   Nimekubali kumfuata Yesu
   Sitarudi nyuma kamwe
2. Baba na mama wakiniacha
   Baba na mama wakiniacha
   Baba na mama wakiniacha
   Sitarudi nyuma kamwe
3. Hata shetani akinguruma
   Hata Shetani akinguruma
   Hata Shetani akinguruma
   Sitarudi nyuma kamwe
4. Rafiki zangu wakinitenga
   Rafiki zangu wakinitenga
   Rafiki zangu wakinitenga
   Sitarudi nyuma kamwe

22. YESU AKIJA TUTAFANYA NINI

1. Yesu akija tutafanya nini x2
   Moyo wangu sikia x2
   Moyo wangu x4
   Moyo wangu sikia x2
2. Dhambi zako umezikumbuka x2
   Kama hivyo utubu x2
   Kama hivyo x2
   Kama hivyo utubu x2
3. Siku ya mwisho tutafanya nini x2
   Ee nduguni tutubu x2
   Ee nduguni x4
   Ee nduguni tutubu x2
4. Je mwenzangu umekuwa tayari x2
   Ikiwa hivyo nifuraha x2
   Ikiwa hivyo x4
   Ikiwa hivyo ni furaha x2

23. NI TABIBU WA KARIBU

1. Ni Tabibu wa karibu
   Tabibu wa ajabu;
   Na rehema za daima
   Ni dawa yake njema

   lmbeni malaika, Sifa za Yesu Bwana
   Pweke limetukuka, Jina lake Yesu

2. Hatufai kuwa hai
   Wala hatutumai
   lla yeye kweli ndiye
   Atupumzishaye.

3. Dhambi pia na hatia
   Ametuchukulia
   Twenendeni na Amani
   Hata kwake Mbinguni

4. Huliona tamu jina
   La Yesu Kristo Bwana
   Yuna sifa mwenye kufa
   Asishindwe na kufa

5. Kila mume asimame
   Sifa zake zivume
   Wanawake na washike
   Kusifu jina lake

6. Na vijana wote tena
   Wampendao sana
   Waje kwake wawe wake
   Kwa utumishi wake.

24. ANGALIA BWANA YESU

1. Ninaleta neno jema la uzima
   Maneno yenye kuokoa
   Kwamba Yesu alifia wenye dhambi
   Angalia Bwana Yesu Kristo

   Angalia Bwana anatuokoa zote
   Nao wanaomwamini wanapona
   Angalia Bwana Yesu Kristo

2. Ninaleta neno jema la uzima.
   Maneno yenye kuokoa
   Kwamba Yesu alifia wenye dhambi
   Angalia Bwana Yesu Kristo

3. Unawezaje kuishi siku hiyo.
   Watu watakapohukumiwa.
   Usimkatae Mwokozi Yesu Kristo
   Anakupenda sana

25. MWAMBA WENYE IMARA

1. Mwamba wenye imara kwako nitajificha!
   Maji hayo na damu yaliyotoka humu.
   Hunisafisha dhambi, Hunifanya mshindi.

2. Kwa kazi zote pia sitimizi sharia
   Nijapofanya bidii, Nikilia na kudhii
   Hayaiishi makosa, ndiwe wa kuokoa

3. Sina cha mkononi, naja msalabani;
   Nili tupu nivike, Ni mnyonge, nishike,
   Nili mchafu naja, Nioshe nisijafa.

4. Nikungojapo chini. Nakwenda kaburini,
   Nipaapo mbinguni, Na kukwona enzini
   Roho yangu na iwe rahani mwako wewe.

26. DAMU IMEBUBUNJIKA

1. Damu imebubunjika
   Ni ya Imanweli
   Wakioga wenye taka
   Husafiwa kweli
2. Ilimpa kushukuru
   Mwivi mautini
   Nami nisiye udhuru
   Yanisafi ndani
3. Kondoo wa kuuawa
   Damu ina nguvu
   Wako wote kuokoa
   Kwa utimilivu
4. Bwana, tangu damu yako
   Kunisafi kale
   Nimeimba sifa zako
   Taimba milele
5. Nikifa tazidi kwimba
   Sifa za wokovu
   Ulimi ujaponyamaa
   Vumbini mwa mfu

27. YESU NI JINA NIPENDALO

1. Yesu ni jina nipendalo
   Na penda kulisikia
   Napenda kulitamka hilo
   Lililonidhihirisha
2. Jina hilo huniambia
   Mwokozi alinipenda
   Damu yake ilimwagika
   Nipate kuokoka

   Yesu, nakupenda
   Yesu, nakupenda
   Yesu, nakupenda
   Kwani ulinipenda
3. Lanionyesha sifa yake
   Iliyo katika Baba
   Njia ijapokua kwa giza
   Yesu huniongoza
4. Lanidhihirisha Yesu
   Aliyenihurumia;
   Laondoa taabu yangu,
   Niwe wake daima

28. BARAGUMU YAKE BWANA

1. Baragumu yake Bwana wakati ikipigwa
   Na siku ya milele ikifika;
   Hapo waliokombolewa watakusanyika
   Nitakuwako, jina kuitika

   Na Majina yaitwapo
   Na majina yaitwapo
   Na majina Yaitwapo
   Kuitika jina, nitakuwapo

2. Wafu wa Kristo wafufukapo kwa siku ile,
   Tutashiriki na fahari yake;
   Waliochaguliwa watakaribishwa kwake
   Nitakuwapo jina kuitika

3. Saa zote na tumfanyie Bwana kazi yake
   Tangu asubuhi hata jioni
   Maisha yetu ikomapo humu duniani
   Nitakuwako jina kuitika

29. AKIITA NITAITIKA

1. Akiita, nitaitika
   Akiita, nitaitika
   Akiita, nitaitika
   Nitasema, Nipo Bwanangu
   Nitasema...Nipo
   Nitasema...Nipo
   Nitasema...Nipo Bwanangu
   Nitasema...Nipo
   Nitasema...Nipo
   Nipo, Yesu, kukusikia.

2. Akiita, nitaitika,
   Akiita, nitaitika,
   Akiita, nitaitika,
   Nitafanya kazi ya Bwana
   Nitafanya..fanya kazi
   Fanya...fanya kazi
   Fanya ...kazi ya Bwana
   Nitafanya...fanya kazi
   Fanya... fanya kazi
   Fanya kazi ya Bwana

30. SITAONA GIZA YESU AJAPO

1. Sitaona giza Yesu ajapo x3
   Kunyakua watu wake.

   Kunyakua watu wake x2
   Sitaona giza Yesu ajapo,
   Kunyakua watu wake.

2. Sitafadhaika Yesu ajapo x3
   Kunyakua watu wake.
3. Sitalia tena Yesu ajapo x3
   Kunyakua watu wake.
4. Nitamkaribisha Yesu ajapo x3
   Kunyakuwa watu wake.

31. AMANI NAIWEKA NYUMBA KWA BWANA YANGU

1. Amani naiweka nyumba kwa Bwana yangu
   Bwana akiwepo na mwenye kupenda Amani
   Nitakuwa naye daima kwa Mungu
   Baba milele na milele

   Mwokozi Yesu tunakuomba tupe Roho
   Mtakatifu, tukumbuke vyote tulivyo
   Navyo ni mall yake Bwana Haleluya
   Asifiwe Bwana Mungu.

2. Tunapoambiwa habari ya imani yake
   Tujinyenyekeze kwa Mungu Baba Mwenyezi
   Nakuweka yote mikononi mwake na halafu atusamehe
3. Tujue upendo unatungojea kwake
   Tukafike mbinguni kwenye imani kweli
   Tusipoteze muda tumfuateni Mungu
   Kwa Iile asemalo

32. BABA MUNGU NAKUSHUKURU

1. Baba Mungu nakushukuru
   Baba Mungu nakushukuru
   Nakupenda, nakusifu, nakusujudia
   Baba Mungu nakushukuru
2. Mwana wa Mungu nakutukuza
   Mwana wa Mungu nakutukuza
   Ulinipa wokovu, uzima ninao
   Mwana wa Mungu nakutukuza

33. NASIKITIKA SANA MOYONI MWANGU

1. Nasikitika sana moyoni mwangu
   Ni nani aliyeniumba mimi? x2

   Ni yeye mwenyezi Mungu
   Ni Bwana Mwenyezi Mungu
   Muumba mbingu na Ulimwengu x2

2. Natangatanga popote duniani
   Ni nani aliyeniumba mimi? x2
3. Watangatanga popote duniani
   Ni nani aliyekuumba wewe? x2
4. Mwili wangu na mifupa yangu yote
   Ni nani aliyeuumba hivyo? x2
5. Mataifa wamchukia Mungu
   Ni nani aliyewaumba hao x2
6. Hata wewe umkatae Mungu
   Ni nani aliyekuumba wewe x2

34. CHOMBO CHAKO

1. Ninakushukuru Bwana
   Kwani uliniokoa
   Vile ulinisafisha
   Niwe chombo chako safi.
2. Chombo tupu unilishe
   Na baraka zako kubwa
   Mito ya maji ya uzima
   Itatoka ndani yangu.

   Chombo chako Bwana Yesu
   Niko Mikononi mwako
   Uyalishe utumie
   Kila siku kila saa.

3. Sina nguvu ila Yako
   Ndiyo Roho yako Mungu
   Uyalishe na uwezo
   Niwe mshuhuda wako.
4. Mimi chombo cha udongo
   Utukuzwe ndani yangu
   Ulinunua Bwana
   Niikale mall yako

35. BABA YETU ALIYE MBINGUNI

1. Baba yetu aliye mbinguni
   Amenifurahisha yakini
   Kuniambia mwake chuoni
   Ya kuwa nami Yesu pendoni.
2. Nimwachapo kutanga mbali
   Yeye yu vivyo hupenda kweli
   Hunirejeza kwake moyoni
   Kweli yu nami Yesu pendoni
3. Anipenda! Nami nampenda
   Kwa wokovu alionitenda
   Akanifia msalabani
   Kwa kuwa nami Yesu pendoni
4. Haya kujua yanipa raha
   Kumwamini kuna furaha
   Humfukuza mara shetani
   Kwona yu nami Yesu pendoni.

5 Sifa ni nyingi asifiwazo
Moja ni sana katika hizo
Wala siachi hata Mbinguni
Kwimba "Yu nami Yesu pendoni."

Anipenda Mwokozi Yesu,
Anipenda, anipenda
Anipenda Mwokozi Yesu,
Anipenda mimi.

36. MJI MZURI

1. Kuna mji mzuri Yerusalem
   Uliopambwa hasa kwa kila rangi
   Uliotayarishwa na kubaliwa
   Na watakaoshinda dhambi milele. x2

   Umejengwa, na Mungu, naye
   Mwana kondoo.
   Ni mji wa raha, shida magojwa na
   Na maombolezo havipo milele.

2. Waliokombolewa toka dhambini
   Watakwenda Mbinguni Yerusalemu
   Watafutwa machozi na mwana kondoo,
   Wataimba Hosana mbele ya Mungu.

3. Katika mji ule Yerualemu
   Hautaingiliwa kamwe na mwovu
   Ole wetu kabisa tusipo shinda
   Hatutakaribishwa Yerusalemu.

37. AMENIITA MWOKOZI

1. Ameniita mwokozi wa upendo,
   Ameniita nitamtumikie
   Kwa furaha nitamtumikia siku moja
   Atanipumizisha

   Ni furaha kwa Bwana Wangu(atanipumzisha)
   Baada ya kazi Duniani, atanipumzisha
   Nitapata uzima wa milele Bwana Yesu
   atanipumzisha

2. Kazi zake mwokozi wa upendo
   Nitafanya mpaka siku ya mwisho
   Watu wote wapate kuokoka
   Watapata uzima wa milele

3. Bwana wangu nitamtumikia
   Kila siku nitamtumikia
   Mpaka watu wapate kuishika
   Nitafanya juhudi waishike

38. NJONI NA FURAHA

1. Njoni na furaha, enyi wa imani,
   Njoni Bethlehemu upesi!
   Amezaliwa jumbe la Mbinguni
   Njoni tumuabudu, Njoni tumabudu,
   Njoni tumuabudu Mwokozi.

2. Mungu wa waungu, Mwanga wa mianga,
   Amekuwa radhi kuzaliwa:
   Mungu wa kweli, wala si kiumbe
   Njoni tumuabudu, Njoni tumuabudu,
   Njoni tumuabudu Mwokozi.

3. Jeshi la mbinguni, Imbeni kwa nguvu!
   Mbingu zote na zijae sifa!
   Sifuni Mungu aliye mbinguni;
   Njoni tumuabudu, Njoni tumuabudu,
   Njoni tumuabudu Mwokozi.

39. KUPIGANA VITA

1. Kupigana vita niko tayari
   Biblia silaha ya vita
   Vita vyake Bwana nitapigana
   Kwa nguvu zake mwokozi.

   (Nipe) Nipe uwezo wako Bwana
   (Niwe) Mshindi wa vitani
   (Nipa) Nipate kumshinda yule
   mwovu shetani.

2. Nguvu za shetani tutazishinda
   Kama tukimwomba Bwana
   Atatupa nguvu tukimshinda
   Tukae naye mwokozi.

3. Kuna raha kule kwa Bwana Yesu
   Yesu ndiye kiongozi
   Tujikaze ndugu kupiga vita,
   Njia yetu ni msalaba.

40. KWA KALVARI

1. Muda mwingi nilipotea
   Sikufahamu msalaba
   Wala aliyenifilia
   Kwa kalvari.

   Rehema bure na neema
   Samaha nalo nilipewa
   Ndipo aliponifungua
   Kwa kalvari.

2. Kwa neno lake Bwana Mungu
   Nilijiona mimi mwovu
   Ni kageuka na kutubu
   Kwa kalvari.

3. Yote kwa Yesu namtolea
   Ndiye mfalme wa pekee sasa
   Kwa furaha nitamwambia
   Kwa kalvari.

4. Jinsi pendo lilivyo kuu
   Neema ilishushwa toka juu
   Alitufanyia wokovu
   Kwa kalvari.

41. MLE KABURINI

1. MIe kaburini, Yesu Mwokozi!
   Alilazwa chini, Bwana wangu!

   Bwana amefufuka! Kifo kimeshindwa kabisa!
   Gizani mle alitoka chini, sasa atawala huko mbinguni
   Yu hal! Yu hai! Bwana Yesu yu hai!

2. Auugoja huo, Yesu Mwokozi!
   Mchana ujao, Bwana wangu!

3. Walinda kaburini, Yesu Mwokozi!
   Bure ni muhuri, Bwana wangu!

4. Kifo kimeshindwa, Yesu Mwokozi!
   Pingu zimevunjwa, Bwana wangu!

42. AWAYE YEYOTE

1. Awaye yote, kama anataka
   Kufuatana nami,
   Ajikane mwenyewe x2

   Yesu anasema, na tukajitwike
   Msalaba wetu ndipo tukamfuate
   (Kwa kuwa mtu atakaye)
   Kuokoa nafsi (yake)
   Ataipoteza (bali)
   Kwa ajill ya Yesu ataiokoa

2. Ni faida gani mtu kuupata
   Ulimwengu wote na mwisho apotee x2

3. Tutatoa nini kwa mwokozi Yesu,
   Kama kazi zote kwa nafsi zetu x2

43. NINA HAJA NAWE

1. Nina haja nawe kila saa:
   Hawezi mwingine kunifaa.

   Yesu nakuhitaji, Vivyo kila saa!
   Niwezeshe Mwokozi, Nakujia,

2. Nina haja nawe; kaa nami,
   Na maonjo haya, Hayaumi.

3. Nina haja nawe: Kila hali,
   Maisha ni bure, Uli mbali.

4. Nina haja nawe, Nifundishe
   Na ahadi zako zifikishe.

5. Nina haja nawe; Mweza yote
   Ni wako kabisa siku zote.

44. TUMESAFISHWA KWA DAMU

1. (Haleluya) Yesu Bwana wetu
   (Haleluya) Yesu Bwana wetu
   Tumesafishwa kwa damu ya Yesu
   Yesu Bwana wetu
2. (Haleluya) tulinunuliwa
   (Haleluya) tulinunuliwa
   Tumesafishwa kwa damu ya Yesu
   Tulinunuliwa.
3. (Haleluya) alituokoa
   (Haleluya) alituokoa
   Tumesafishwa kwa damu ya Yesu
   Alituokoa.
4. (Haleluya) twaitwa Wakristo
   (Haleluya) twaitwa Wakristo
   Tumesafishwa kwa damu ya Yesu
   Twaitwa wakristo.
5. (Haleluya) twaishi na Kristo
   (Haleluya twaishi na Kristo
   Tumesafishwa kwa damu ya Yesu
   Twaishi na Kristo.
6. (Haleluya) tu wana wa Mungu
   (Haleluya) tu wana wa Mungu
   Tumesafishwa kwa damu ya Yesu
   Tu wana wa Mungu.
7. (Haleluya) Shetani ashindwe
   (Haleluya) Shetani ashindwe
   Tumesafishwa kwa damu ya Yesu
   Shetani ashindwe.

45 HUKUMU INAKUJA

1. Hukumu inakuja ndugu yangu,
   Ujihadhari na dunia hii;
   Ni wakati kidogo umebaki,
   Dunia hii iwake moto. x2

   Watallalialia, na kusaga meno
   Watallalialia, na kuomboleza
   Watallalialia, na kusaga meno
   Na hawatasamehewa.

2. Hakuna usalama siku hizi
   Kila pahali nipa hatari
   Ni wakati kidogo umebaki
   Dunia hii iwake moto x2

3. Uaji, umezidi ndugu yangu
   Ulevi na unyang'anyi pia
   Ni wakati kidogo umebaki
   Dunia hii iwake moto x2

46. USIKU MKUU!

1. Usiku mkuu! Mtakatifu! Uko utulivu.
   Birika amezaa Mwana. Mtoto Mtakatifu ni Bwana
   Alale amanini, Alale amanini

2. Usiku mkuu! Mtakatifu! Wachungwa wa hufu,
   waliogopa kuwaona, Malaika walipoimba
   Kristo amezaliwa, Kristo amezaliwa.

3. Usiku mkuu! Mtakatifu! Ni Mwana wa Mungu.
   Ametutetea neema, ili tukae na salama.
   Yesu Kristo Mwokozi, Yesu Kristo Mwokozi

47. BWANA MUNGU MTAKATIFU

1. Ewe Bwana Mungu Mtakatifu
   Uwezo wako umezidi vyote X2

   Ni ya ajabu Baba Mtakatifu
   Kwa mapenzi yako ewe Bwana x2
   Bwana uniandike name
   Katika kitabu chako mbinguni x2

2. Utukufu wako ewe Bwana
   Umezidi vyote ulimwenguni x2
3. Ufalme wako ewe Bwana
   Umezidi vyote ulimwenguni x2
4. Damu yako msalabani
   Mwokozi wetu amezidi vyote x2
5. Uzima wako ewe Bwana
   Umezidi vyote ulimwenguni X2

48. SIMAMA IMARA

1. Milima yote na mabonde itayeyuka,
   Neno lake Bwana imara litasimama.

   (Simama) simama imara jilinde
   Neno lake Bwana imara
   Kesha kila siku uombe
   (Uombe) utasimama x2

2. Mapendo ya Mungu tumejaa, Roho wa kweli, Imara yetu ndani yake,
   Awe muhuri.
3. Siku za huduma ni chache tuwe mashujaa
   Roho wa Yesu akae nasi, mpaka hatima
4. Katika yote tutashinda kwa nguvu zake,
   Nani aweza kututenga, na pendo lake.

49. WANDUGU NA WADADA

1. Wandugu zetu na wadada wote
   Jihadhari siku inayokuja
   Siku ile isiyojulikana
   Ila Mungu pekee ajuaye.

   Wenye dhambi, wote watalia, Watakapotupwa motoni
   Watalia woi, woi, woi, woi, woi, woi kama tungejua

2. Waliokoka watapokelewa
   Kwa imani watamtumikia
   Bwana Yesu atawakaribisha
   Kwa ulinzi wa ufalme wa Mbinguni.

3. Watu watatoa visababu
   Wengine watasema ni Wahubiri
   Wengine watasema ni wa kanisa
   Na Mungu Baba hatawasikiliza.

4. Wahubiri walihubiri
   Biblia inasema wazi
   Jihadhari miango utafungwa
   Ukibisha utafunguliwa.

50. KAZI YANGU IKIISHA

1. Kazi yangu ikiisha, nami nikiondoka,
   Na kuvaa kutokuharibika,
   Nitamjua Mwokozi nifikapo ng'amboni,
   Atakuwa wa kwanza kunilaki.

   Nitamjua, nitamjua nikimwona uso kwa uso,
   Nitamjua, nitamjua kwa alama za misumari

2. Furaha nitapata nikiona makao
   Bwana aliyotuandalia
   Nitamsifu Mwokozi kwa rehema na pendo
   Vilivyonipa pahali Mbinguni

3. Nao waliokufa katika Bwana Yesu
   Nitawaona tena huko juu
   Lakini nifikapo kwake huko Mbinguni
   Nataka kumwona Mwokozi kwanza.

4. Mitangoni mwa mji Bwana atanipisha
   Pasipo machozi wala huzuni
   Nitaimba wimbo wa milete; lakini
   Nataka kumwona Mwokozi kwanza

51. NDIYO DHAMANA YESU WANGU

1. Ndiyo dhamana Yesu wangu
   Hunipa furaha ya Mbingu
   Mrithi wa wokovu wake
   Nimejawa kwa Roho yake.

   Habari njema raha yangu
   Yesu ndiye mwokozi wangu
   Habari njema raha yangu
   Yesu ndiye mwokozi wangu

2. Kumsalimu moyo wangu
   Mara namwona raha yangu
   Aniletea malaika
   Wananilinda taokoka.

3. Sina kinyume nashukuru
   Mchana kutwa huja kwangu
   Usiku kucha kuna nuru
   Mwokozi wangu ndimi nuru.

4. Halil na mali anitwaa
   Mara namwona anifaa
   Nami nangoja kwa subira
   Akiniita nije mara.

52. TANGAZA MILIMANI

1. Tangaza milimani habari za wokovu
   Wakidhani ni uongo Yesu atatokea x2

   (Ndugu) Ujiulize nami nijiulize
   (Dada) Ujiulize nami nijiulize
   (Baba) Ujiulize nami nijiulize
   (Sote ikiwa tunamgojea Bwana)

2. Yesu atakaporudi chini mara ya pili
   Wale watakatifu wataona furaha x2

3. Yesu atawatenga kondoo na mbuzi,
   Kondoo kuume na mbuzi kushoto x2

4. Wengi watamwomba twataka kutubu
   Bwana atawajibu wakati umekwisha. x2

5. Sasa ndio wakati wetu wa kutubu.

Tukidhani ni uongo yeye atatokea x2

53. MEZA YA BWANA

1. Kila Jumapili tukumbuke
   Kila Jumapili tukumbuke

   Bwana alivyosema tukumbuke
   Kumbuka kumbuka tukumbuke (x2)

2. Tule mwili wa Yesu tukumbuke
   Tule mwili wa Yesu tukumbuke
3. Tunywe damu ya Kristo tukumbuke
   Tunywe damu ya Kristo tukumbuke
4. Twende kanisa la Kristo tukumbuke
   Twende kanisa la Kristo tukumbuke
5. Tusome injili ya Yesu tukumbuke
   Tusome injili ya Yesu tukumbuke

54. DAMU YA YESU

1. Damu ya Yesu x3
   Husafisha kabisa
2. Yesu ndiye njia ya uzima x3
   Asifiwe Mwokozi
3. Sisi tunaimba haleluya x3
   Asifiwe Mwokozi
4. Yesu ndiye Alfa na Omega x3
   Asifiwe Mwokozi
5. Tumevikwa taji ya uzima x3
   Asifiwe Mwokozi
6. Siku Moja Yesu atarudi x3
   Asifiwe mwokozi
7. Nguvu za Shetani zimeshindwa na Yesu x3
   Asifiwe Mwokozi
8. Milele tutaimba Haleluya x3
   Asifiwe Mwokozi

55. NIMEPATA NJIA

1. Nimepata njia, njia, njia
   Nimepata njia, njia, njia ya uzima
2. Nimepata ukweli, ukweli, ukweli
   Nimepata ukweli, ukweli wa uzima
3. Nimepata ngao, ngao, ngao
   Nimepata ngao, ngao ya uzima
4. Na Yesu ndiye njia, njia, njia
   Na Yesu ndiye njia, njia ya uzima

56. ENEZA HABARI

1. Eneza habari humu duniani
   Popote panapo moyo wa huzuni
   Ndimi za Wakristo zitangaze
   neno, yupo mfariji.

   Yupo mfanji, yupo mfanji
   Roho mtakatifu ndiye msaidizi
   Eneza habari humu duniani
   Yupo mfanji.

2. Mfalme wa wafalme, Yesu utazame
   Ametuletea sifa ya milele
   Mateka wapate ukombozi wake,
   Yupo mfariji
3. Niwezeje mimi kutamka vizuri
   Kumsifu Mwokozi aliye mbinguni
   Nitangaze sasa, neno la furaha
   Yupo mfariji.
4. Wenzangu tuimbe nyimbo za milele
   Mbinguni tujaze na shukrani tele
   Upendo wa Bwana ujulike sasa
   Yupo mfariji.

57. BWANA MUNGU, NASHANGAA

1. Bwana Mungu, na shangaa kabisa
   Nikitazama kama vilivyo
   Nyota ngurumo vitu vingi vyote
   Viumbavyo kwa uwezo wako

   Roho yangu na ikuimbie, Jinsi wewe ulivyo mkuu
   Roho yangu na ikuimbie, Jinsi wewe ulivyo mkuu

2. Nikitembea pote duniani
   Ndege huimba nawasikia
   Milima hupendeza macho sana
   Upepo nao nafurahia

3. Nikikumbuka kama wewe Munoy
   Ulivyompeleka mwanao
   Afe azichukue dhambi zetu
   Kutambua ni vigumu mno

4. Yesu Mwokozi utakaporudi
   Kunichukua kwenda mbinguni
   Nitashukuru na kwimba milele
   Wote wajue jinsi ulivyo

58. NIONAPO MTI BORA

1. Nionapo mti bora, Kristo aliponifia
   Kwangu pato ni hasara
   Kiburi nakichukia.

2. Na nisijivune, Bwana,
   Ila kwa mauti yako;
   Upuzi sitaki tena,
   Ni chini ya damu yako

3. Tangu kichwa hata nyayo
   Zamwagwa pendo na hamu
   Ndako pweke hamu hiyo,
   Pendo zako zimetimu.

4. Vitu vyote vyo dunia,
   Si Sadaka ya kutosha,
   Pendo zako zaniwia
   Nafsi, mali, na maisha.

59. KARIBU NAWE, EE MWOKOZI

1. Karibu nawe, Ee Mwokozi,
   Univute Bwana wa thamani;
   Unikaribishe moyoni,
   Uniweke kwako salamani,
   Uniweke kwako salamani.
2. Karibu nawe, sina kitu,
   Sikuiletea sadaka kuu;
   Nakujitolea kabisa,
   Kwa damu nipate kutakaswa,
   Kwa damu nipate kutakaswa.
3. Karibu nawe, Bwana wangu,
   Niliuacha uovo wangu;
   Kiburi changu na anasa,
   Namtaka Yesu aliye Bwana,
   Namtaka Yesu aliye Bwana.
4. Karibu nawe, hata mwisho,
   Nina salama ndani ya Kristo
   Mwokozi wangu kwa milele,
   Nitakuwa karibu na wewe,
   Nitakuwa karibu na wewe.

60. PANDA ASUBUHI

1. Panda asubuhi mbegu ya fadhili
   Panda adhuhuri, tena jioni
   Tutaingojea siku ya mavuno
   Tutafurahi kuleta mavuno

   Leta mavuno, Ieta mavuno
   Tutafurahi kuleta mavuno
   Leta mavuno, Leta mavuno
   Tutafurahi kuleta mavuno

2. Na panda mwangani, tena kivulini
   Usiwe na hofu kwa baridi mkuu
   Na mwisho wa kazi kuvuna mavuno
   Tutafurahi kuleta mavuno
3. Mvunieni Bwana kwa machozi mengi
   ljapo twaona taabu nyingi
   Mwisho wa kilio tutakaribishwa
   Tutafurahi kuleta mavuno

61. USINIPITE MWOKOZI

1. Usinipite Mwokozi
   Unisikie
   Unapozuru wengine
   Usinipite

2. Kiti chako cha rehema
   Nakitazama
   Magoti napiga pale
   Nisamehewe

   Yesu, Yesu Unisikie
   Unapozuru wengine, Usinipite

3. Sina cha kutegemea
   lla wewe tu
   Uso wako uwe kwangu
   Nakuabudu

4. U mfariji peke yako
   Sina Mbinguni
   Wala duniani pote
   Bwana mwingine

62. TWONANE MILELE

1. Nyimbo na tuziimbe tena
   Za alivyotupenda mbele
   Kwa damu ya dhamani sana
   Mbinguni hwonana milele

   Twonane milele, Twonane bandarini kule
   Twonane milele, Twonane bandarini kule

2. Hupozwa kila aoshwaye
   Kwa damu ya Kondoo yule
   Ataishi afurahiye
   Vya Yesu Mbinguni milele

3. Hata sasa hufurahia
   Tamu yake mapenzi yale
   Je, kwake tukifikilia
   Kutofarakana milele?

4. Twende mbele kwa jina lake
   Hata aje mwokozi yule
   Atatukaribisha kwake
   Tutawale naye milele

5. Sauti zetu tuinue
   Kumsifu Mwokozi yule
   Ili watu wote wajue
   Wokovu u kwake milele

63. YESU MPONYA

1. Yesu mponya Bwana wangu
   Uchukue roho yangu
   Niishipo duniani
   Naishi majaribuni

   Uchukue roho yangu Bwana
   Unilinde Yesu mponya Bwana
   Uniongoze mbinguni
   Nyumbani mwa Baba Mungu

2. Ulikufa kwa kalvari
   Ulifia wenye dhambi
   Damu yako ilimwagwa
   Kwa kutulipia deni

3. Machafuko na Mabaya
   Majaribu hapa chini
   Utuhurumie Yesu
   Yesu Bwana wa salama

64. MJI WA YERUSALEMU

1. Mji wa Yerusalemu umetayarishwa sana
   Milango kumi na mbili ya watu wa Mungu
   Imeandikwa majina ya wateule wake Mungu
   Majina hayo kabila ya Waisraeli.

   Upande—upande wa mashariki milango mitatu
   Upande...upande wa magharibi milango mitatu
   Kusini... Kaskazini mitatu mitatu
   Zingatia kabila ya Waisraeli

2. Yesu atakaporudi kuchukua wateule
   Wengine watakimbia tena siku hiyo
   Majeshi ya mia moja arobaini na nne elfu
   Wataimba haleluyah na mwana kondoo.

65. HAKUNA RAFIKI

1. Hakuna rafiki kama Yesu,
   Yu pekee, yu pekee,
   Hakuna mpozi kama Yesu
   Yu pekee, Yu pekee.
2. Yeye anaye sifa, ni Yesu
   Yu pekee, Yu pekee
   Ndiye aliye mnyenyekevu
   Yu pekee, Yu pekee
3. Yesu pamoja nasi daima
   Yu pekee, Yu pekee
   Kwa usiku aleta salama
   Yu pekee, Yu pekee
4. Kulinda Yesu ni mwaminifu
   Yu pekee, Yu pekee
   Atakubali watakatifu
   Yu pekee, Yu pekee

Yesu ajua shida zetu, Aweza kutongoza;
Hapana rafiki kama Yesu, Yu pekee, Yu pekee

66. NAENDEA MSALABA

1. Naendea msalaba
   Ni mnyonge na mpofu
   Yapitayo naacha
   Nipone Msalabani
2. Nakulilia sana
   Nalemewa na dhambi
   Pole Yesu asema
   Nitazifuta zote
3. Natoa vyote kwako
   Nafasi nazo nguvu
   Roho yangu na mwili
   Viwe vyako milete
4. Kwa damu yake sasa
   Nimegeuka roho
   Nikaziacha tamaa
   Nimfuate Yesu

Nakutumani tu,
Ewe Mwana wa Mungu
Nainamia kwako
Niponye, mponya wangu

67. KUMTEGEMEA MWOKOZI

1. Kumtegemea Mwokoz
   Kwangu tamu kabisa
   Kukubali neno lake
   Nina raha moyoni

2. Kumtegemea Mwokozi
   Kwangu tamu kabisa
   Kuamini damu yake
   Nimeoshwa kamili

   Yesu, Yesu namwamini
   Nimemwona dhabiti
   Yesu, Yesu Yu dhamani
   Ahadi zake kweli

3. Kumtegemea Mwokozi
   Kwangu tamu kabisa
   Kwake daima Napata
   Uzima na amani

4. Nafurahi kwa sababu
   Nimekutegemea;
   Yesu, Mpendwa na Rafiki
   Uwe nami dawamu

68. MIMI NDIYE WA KWANZA

1. Mimi ndiye wa mwanzo,
   Tena na wa mwisho,
   Usiwe naye Mungu,
   Mwingine kabisa.
   Ndivyo anavyosema
   Baba wa majeshi
   Mungu mtakatifu
   Mwenye nguvu zote.

   Mimi nitampa (yule)
   Ahadi ya uzima (bure)
   Yule atakayeshinda ya dunia hayo (yote)
   Atakuwa ndani yangu
   Hata mimi, ndani yake
   Kwenye utukufu ule
   Wataimba juu mbinguni

2. Mimi nilikuumba unitumikie
   Katika siku zote hapa duiani,
   Mbona sasa waacha njia ile nzuri,
   Wamfuata shetani atakupoteza.

3. Acha udanganyifu twende kwake sasa
   Yeye ni wa rehema tena wa upole,
   Machozi yetu yote yeye atafuta
   Tutakapomwendea na kutubu kweli.

69. FURAHA KWA ULIMWENGU

1. Furaha kwa ulimwengu! Bwana amekuja.
   Nyote Mkaribisheni, moyo yenu na mpeni.
   Wote wamshangilie, Wote wamshangilie,
   na wote, na wote wamshangilie.

2. Furaha kwake dunia! Mwokozi ni Mfalme.
   Bonde na mlima na mwamba, maji mtoni na shamba
   Rudisheni sauti, Rudisheni sauti
   Rudisheni, na rudisheni sauti.

3. Dhambi zisiongezeke, wala wahalifu;
   Yuaja kutubariki, Atuletea ushindi,
   Kuharibu dhambi, Kuharibu dhambi
   Na kuharibu, na kuharibu dhambi

4. Atawala na neema, Kwao mataifa;
   Utukufu na waone, Haki yake itendeke;
   Kwa upendo wake, Kwa upendo wake
   Kwa upendo, na kwa upendo wake

70. WAIMBA SIKIZINI

1. Waimba, sikizeni, Malaika mbinguni,
   Wimbo wa tamu sana, wa pendo zake Bwana,
   "Duniani salama, Kwa wakosa rehema"
   Sisi sote na twimbe, nao wale wajumbe,
   Waimba, sikizeni, Malaika mbinguni

2. Ndiye Bwana wa mbingu, Tangu milele Mungu,
   Amezaliwa mwili, Mwana wa mwanamwili;
   Ametoka enzini, Kuja ulimwenguni
   Mwokozi atufie, ili tusipotee
   Waimba, sikizeni, Malaika mbinguni.

3. Seyidi wa amani, Ametoka mbinguni,
   Jua na haki, ndiye atumulikiaye
   Amejivua enzi, Alivyo na mapenzi
   Ataka kutuponya, Kutuzalisha upya,
   Waimba, sikizeni, Maliika mbinguni

4. Njoo upesi, Bwana, Twakutamani sana;
   Kaa nasi, Mwokozi, Vita hatuviwezi,
   Vunja kichwa cha nyoka, Sura zako andika,
   Tufanane na Wewe, Kwetu sifa upewe
   Waimba, sikizeni, Malaika mbinguni.

71. YESU ATAKA KIANGA

1. Yesu ataka kianga,
   Kung'ara daima
   Kwa Yesu niwe kianga
   Po pote daima
2. Niwe mpenzi wa Yesu
   Niwapende wote;
   Kuwaonyesha wengine
   Pendo siku zote

   Kianga, Kianga
   Kwa Yesu niwe kianga
   Kianga, kianga
   Niwe kianga kwake

3. Bwana Yesu, nimwulize
   Anisaidie
   Moyo wangu utakaswe
   Naye siku zote
4. Niwe kianga kwa Yesu
   Kuwa mwaminifu;
   Nitumike naye Yesu
   Kisha nitamsifu

72. TWENDE KWAKE

1. Twende kwake, twende kwake, kwake Yesu sasa,
   Sasa twende kwake, kwake Yesu sasa!
2. Akwokoe, akwokoe, Bwana Yesu sasa!
   Sasa akwokoe, Bwana Yesu sasa!
3. Anaweza anaweza, Bwana Yesu sasa
   Sasa anapenda Bwana Yesu sasa!
4. Msadiki, msadiki, Bwana Yesu sasa,
   Sasa msadiki, Bwana Yesu sasa!
5. Anapenda, anapende Bwana Yesu, sasa
   Sasa anapenda, Bwana Yesu sasa!
6. Njoo hima, njoo hima, kwake Yesu sasa
   Sasa njoo hima, kwake Yesu sasa

73. TOKA UTUMWANI

1. Toka utumwani ninasafiri kila
   Siku, niingie Kanaani
   Niliyoahidiwa, Tuimbe haleluya
   Kweli tumefunguliwa na
   Kwenda Kanaani, Kanaani ya kweli

   Daima nakwenda huko niingie, Kanaani
   Niingie Kanaani niliyoahidiwa, Tuimbe Haleluya
   Kweli tumefunguliwa na enda
   Kanaani, Kanaani ya kweli x2

2. Toka Misri napitia kwenye
   Giza katika milima mabonde
   Jangwa bali sitachoka kamwe
   Bwana ndiye nguvu zangu
   Na kwenda Kanaani, Kanaani ya kweli

3. Niliyotafuta yote niliyoahidiwa
   Nifike Kanaani nchi ya ahadi kwa furaha
   Nitaimba nikimsifu Yesu
   Nakwenda Kanaani, Kanaani ya kweli

74. MWAMINI YESU

1. Mwamini Yesu ni mwokozi
   Aliyeteseka kwako,
   Akapigwa misumari
   Kwa ajili ya dhambi zetu

   Leo tunayo furaha, Kufufuka kwake Yesu mwokozi
   Kumbukumbu hilo Bwana, Ndugu zangu njoo hima.

2. Danieli kweli aliwekwa
   Kwenye shimo walimo simba
   Wala simba hawakumdhuru
   Kwa ajili ya imani

3. Sasa Yesu ndiye njia
   Kwa wachunga wenye imani
   Takataka watakwenda, kwenye moto
   Usio na mwisho,

75. NIONGOZE, BWANA YESU

1. Niongoze, Bwana Mungu,
   Ni msafiri chini,
   Ni mnyonge, nguvu sina
   Nishike mkononi;
   U mkate wa mbinguni
   Nilishe siku zote
   Nilishe siku zote

2. Kijito cha maji mema
   Kitokacho mwambani
   Nguzo yako, moto wingu
   Niokoe Mwenye nguvu
   Nguvu zangu na ngao
   Nguvu zangu na ngao

3. Nikikaribia kufa,
   Sichi neno lo lote
   Wewe kifo umeshinda
   Zinawe nguvu zote
   Tutaimba sifa zako
   Kwako juu milele
   Kwako juu milele

76. NIMELEMEWA NA HATIA ZANGU

1. Nimelemewa na hatia zangu
   Nakutamani kufikia mbingu
   Ingawa mwenye dhambi haingii
   Iko sauti yaniita nije.

   Naja kwako Yesu Bwana
   Nisafiwe dhambi zangu x2

2. Mimi mchafu nitaweza wapi
   Kufika kwenye nchi takatifu
   Kitini kwa mwamuzi ni simame
   Uko mkono wanivuta nije.

3. Ingawa natamani kuifuata
   Njia ya haki dhambi zanipinga
   Lakini nasikia neno njema
   Tubu ungama utasemehewa.

4. Sauti yako Yesu nasikia
   Mikono yako yanivuta leo
   Na damu yako yanisafisha dhambi
   Na kuniweka safi mbete yako.

77. MUNGU NI PENDO

1. Mungu ni pendo, apenda watu
   Mungu ni pendo, anipenda

   Sikilizeni furaha yangu
   Mungu nipendo anipenda

2. Nalipotea katika dhambi
   Nikawa mtumwa wa shetani

3. Akaja Yesu kunikomboa
   Yeye kanipa kuwa huru

4. Sababu hii namtumikia
   Namsifu Yeye siku zote

78. WACHUNGA WALIPOLINDA

1. Wachunga walipolinda, kucha nyama zao,
   Malaika mtukufu, Alishuka kwao
   Wakacha sana wachunga, Akawatuliza,
   "Nawaletea habari ya kupendeza".

2. " Mji ule wa Daudi, Leo amezawa
   Mwokozi, ni Kristo Bwana, Iivyoandikwa:
   Huyo Mwana wa mbinguni, Ataonekana,
   Amelazwa kihorini, Malazi hapana".

3. Alipokwisha yanena, Malaika hao
   Waliimba wimbo huu, Usio na mwisho;
   "Enzi ni yake Mungu juu. Na nchi salama,
   Kwa watu nao radhi kuu, Sasa na daima".

79. NYUMBA YA BABA

1. Twende zote juu nyumba ya Baba
   Nyumba ya Baba, Nyumba ya Baba x2
   Kwenye furaha, furaha, furaha

2. Tutamwona Yesu juu nyumba ya Baba
   Nyumba ya Baba, Nyumba ya Baba x2
   Kwenye furaha, furaha, furaha

80. WAISRAELI KUTOKA MISRI

1. Watu wote shangilia
   Mshukuruni Mungu
   Shangilia mataifa
   Kwa yeye mponya kweli

2. Ndio Waisraeli
   Wanatoka Misri
   Wataka kwenda Kanaani
   Waliko ahidiwa

   (Wali) walifika bahafini
   (Wali) waliona adui wakija
   (Wali) walilalamika sana
   (Naku) nakulia kwa Musa
   (Wali) walilalamika sana
   (Naku) nakulia kwa Musa

3. Jamani tukumbuke kwamba
   Siku hizi za mwisho
   Tusihangaike sana
   Kama wale Wayuda

4. Mungu alionyesha nguvu
   Kakausha bahari
   ligawanyika kati
   Wakapona Wayuda

81. MATAIFA WATAKUSANYA

1. Mataifa watakusanyana
   Mbele yake Yesu Mwokozi
   Mataifa watakusanyana
   Mbele yake Yesu Mwokozi

2. Nikilio kwa wale wote
   Wa mkono wake wa kushoto
   Nikilio kwa wale wote
   Wa mkono wake wa kushoto

3. Aliahidi kuwalinda
   Watakatifu mpaka siku hiyo
   Aliahidi kuwalinda
   Watakatifu mpaka siku hiyo

4. Atahukumu kila mmoja
   Kulingana na matendo yake
   Atahukumu kila mmoja
   Kulingana na matendo yake

   Itika... Yesu wangu
   Itika... Yesu wangu
   Taja.. Yesu
   Tamka... Yesu

82. MWOKOZI WETU NI MWAMBA

1. Mwokozi wetu ni mwamba
   Nikimbilio la kweli
   Halingani na wengine
   Nikimbilio Ia kweli
2. Hata mbele ya kaburini
   Nikimbilio la kweli
   Halingani na wengine
   Nikimbilio la kweli.
3. Alikufa msalabani
   Nikimbilio Ia kweli
   Akazikwa kaburini
   Nikimbilio Ia kweli
4. Alitoka kaburini
   Nikimbilio la kweli
   Akazikwa kaburini
   Nikimbilio Ia kweli
5. Tusiache mwamba wetu
   Nikimbilio Ia kweli
   Yesu ndiye mwamba wetu
   Nikimbilio Ia kweli

Oh Yesu ni mwamba huku duniani
Mwamba huku duniani
Mwamba huku duniani
Oh Yesu ni mwamba huku duniani
Nikimbilio la kweli

83. MILIMA NA MABONDE

1. Kuna milima njiani kuna milima —ooh kuna milima njiani ooh milima na mabonde x2

   Kuna milima njiani kuna milima
   Kuna milima njiani ooh milima na mabonde

2. Uongo pia ni milima uchawi wote ni milima
   Kuna milima njiani ooh milima na mabonde x2
3. Ulati pia ni milima uzinzi pia ni milima
   Kuna milima njiani ooh milima na mabonde
4. Dada yangu kaza mwendo uingie paradise
   Kuna milima njiani ooh milima na mabonde
5. Ndugu yangu kaza mwendo uingie paradise
   Kuna milima njiani ooh milima na mabonde

84. JINA LAKE IMANUELI

1. Jina lake Imanueli
   Mungu pamoja na Wanadamu
   Jina lake Imanueli
   Mungu pamoja na wanadamu
   Aokoa, aokoa kwa ajabu
   Aokoa, kwa ajabu
   Aokoa, kwa ajabu
   Mungu mwenye nguvu
   Anaponya kwa ajabu
   Mungu Mwenye nguvu
   Jina lake ni Imanueli
   Mungu pamoja na wanadamu

85. SIOSHWI DHAMBI ZANGU

1. Sioshwi dhambi zangu
   Bila damu yake Yesu
   Hapendezewi Mungu
   Bila damu yake Yesu.

2. La kunisafi sina
   Ila damu yake Yesu
   Wala udhuru tena
   Ila damu yake Yesu

   Hakuna kabisa
   Dawa ya makosa
   Ya kututakasa
   Ila damu yake

3. Sipati patanishwa
   Bila damu yake Yesu
   Hukumu yaniitisha
   Bila damu yake Yesu

4. Twaimba; utukufu
   Una damu yake Yesu
   Mitele twaisifu
   Hiyo damu yake Yesu

86. YESU MSALABANI

1. Eloi, Eloi lama sabakthani?
   Mungu wangu, mbona umeniacha
   Wahurumie hawana fahamu
   Roho Mtakatifu awajie x2

   Mwana wa..kondoo ndiye kiongozi
   Mwana wa..kondoo ndiye kiongozi
   Eloi...pata mateso mengi
   Eloi...pata mateso mengi
   Eloi... hmmm hmmm hmmm
   Eloi... hmmm hmmm hmmm
   Yesu...alitufia wanyonge
   Yesu...alitufia wanyonge

2. Huyu ndiye mteule wangu
   Aliye kufa akafufuka
   Mariam, Salome na Magdalene
   Walifika huko kaburini. x2

3. Huyu ndiye mlinzi wangu
   Anatulinda siku zote
   Analisha roho zetu pia
   Kwa neno lake takatifu mno x2

87. HARUSI (NDOA) MTAKATIFU

1. Twawapa mafunzo, kwa ndugu na dada
   Watakao unganishwa pamoja x2

   Neema ya Bwana Yesu mwokozi
   lkae nanyi milele
   Mungu azidi kuwabarikia
   Awe ngao yenu na mlinzi wenu x2

2. Mlivyopendana hapo mbeleni
   Mzidi kupendana hata maishani mwenu x2

3. Nawe ndugu mpendwa, mpende mwenzio
   Atakayekuwa ubavuni mwako. x2

88. TWAMSIFU MUNGU

1. Twamsifu Mungu kwa Mwana wa pendo
   Aliyetufilia na kupaa juu

   Aleluya, Usifiwe
   Aleluya, Amina
   Aleluya, Usifiwe
   Utubariki

2. Twamsifu Mungu kwa Roho Mtukufu
   Ametufunulia mwokozi wetu

3. Twamsifu Mwana aliyetufia
   Aliyetwaa dhambi akazifuta

4. Twamsifu Mungu wa neema yote
   Ametukomboa akatuongoza

5. Tuamshe tena tujaze na pendo
   Na moyoni uwashe moto wa Roho

89. SASA NDIO WAKATI

1. Sasa ndio wakati wa kutoa sadaka
   Kila mtu aanze kujifikiria

   Toa ndugu, toa dada x2
   Ulicho nacho wewe
   Bwana anakuona
   Mpaka moyoni mwako.

2. Wiki nzima Bwana Mungu alikulinda vyerna
   sasa nawe ndugu yangu ujifikirie

3. Kumbuka jinsi Yesu alivyojitolea
   Pale msalabani kwa ajili yetu

4. Tolea moyo wako pia matendo yako
   Naye Bwana Mungu atakubariki

5. Baraka zake Mungu, za Baba na za Mwana
   Za Roho Mtakatifu zikae nanyi nyote

90. YOTE NAMTOLEA YESU

1. Yote namtolea Yesu, nampa moyo wote
   Nitampenda siku zote, Namwandama kila saa

   Yote kwa Yesu, Yote kwa Yesu
   Yote kwako Ee Mwokozi, Na toa sasa.

2. Yote namtolea Yesu, nainamia pake

Nimeacha na anasa kwako Yesu nipokee

3. Yote namtolea Yesu, Nifanye niwe wako.
   Nipe Roho yako Bwana, Anilinde daima.

4. Yote namtolea Yesu, Nami naona sasa
   Furaha ya ukombozi, Nasifu jina lake.

91. SI DAMU YA NYAMA

1. Si damu ya nyama
   lliyomwagika
   lwezayo kuondoa
   Dhambi za wakosa

2. Yeye Bwana Yesu
   Sadaka ya Mungu
   Mwenye damu ya thamani
   Ni Mwokozi kweli

   Bwana Yesu ndiye
   Mwokozi wa kweli
   Tumsifu siku zote
   Twapata uhuru

3. Kwa Imani yangu
   Namshika Yeye
   Naziweka dhambi zangu
   Juu ya kichwa chake

4. Mzigo wa dhambi
   Sichukui tena
   Ameauchukua Yeye
   Juu msalaba.

92. NI SIKU KUU

1. Ni siku kuu siku ile
   Ya kumkiri Mwokozi
   Moyo umejaa tele
   Kunyamaza hauwezi

2. Tumekwisha kupatana
   Mimi wake, yeye wangu
   Na sasa nitamwandama
   Nikiri neno la Mungu

   Siku kuu, siku kuu
   Ya kuoshwa dhambi zangu kuu
   Hukesha na kuomba tu
   Ananiongoza miguu
   Siku kuu, siku kuu
   Ya kuosha dhambi zangu kuu

3. Moyo tulia kwa Bwana
   Kiini cha raha yako
   Huna njia mbili tena
   Yesu ndiye njia yako

4. Nadhiri yangu ya mbele
   Nitaiweka daima
   Hata ije siku ile
   Ya kuonana kwa salama

93. ASALI YA NYUKI

1. Asali ya nyuki, mwambani
   Yesu ni kama asali ya nyuki
   Njoo uonje, tamu sana,
   Yesu ni kama asali ya nyuki.

   Na vijana njoo muonje....
   Na wazee….
   Na wamama….

94. NIMECHOKA NAZO DHAMBI

1. Nakujia ni mwenye dhambi
   Nipokee kwa pendo lako
   Nakujia ni mwenye dhambi
   Nipokee kwa pendo lako

   (Yesu) Nimechoka nazo dhambi
   (Bwana) Bwana Yesu nipokee
   (Yesu) Nimechoka nazo dhambi
   (Bwana) Bwana Yesu nipokee

2. Ulipigwa na misumari
   Kwa ajili ya dhambi zetu
   Ulipigwa na misumari
   Kwa ajili ya dhambi zetu

3. Damu yako ilimwagika
   Kwa ajili ya dhambi zetu
   Damu yako ilimwagika
   Kwa ajili ya dhambi zetu

4. Ulikufa msalabani
   Ukateswa na Wayahudi
   Ulikufa msalabani
   Ukateswa na Wayahudi

5. Ulipaa juu mbinguni
   Kutuandalia makao
   Ulipaa juu mbinguni
   Kutuandalia makao

95. ATAKUJA, ATAKUJA

1. Atasanya, Atasanya
   Vito vikusanywe
   Vito vyote vya dhamani
   Wapenzi wake

2. Atachanga, atachanga
   Vito kwa ufalme
   Vito vyote vya dhamani
   Wapenzi wake

3. Ni watoto, ni watoto
   Waitwao vito
   Ni vito vya Yesu Kristo
   Wapenzi wake

   Kama nyota za mbingu
   Wataang'ara kwa Mungu
   Wapenzi ni watoto
   Kwa taji yake

96. NITAKUWA WAPI YESU AKIJA

1. Roho yangu, nataiweka wapi?
   Bwana Yesu akirudi
   Tumwombe Bwana, atuongoze
   Tupate kufika kwake

   Ee ndugu - Njoo, njoo kwa
   Bwana Yesu,
   Nawe utasamehewa
   Ee dada - njoo, njoo kwa
   Bwana Yesu
   Nawe utasamehewa

2. Tujitoe, kweli, kweli
   Tukaihubiri injili
   Miaka ndiyo hii iliyokubaliwa
   Ya kuhubiri injili

3. Bwana akirudi, atatuuliza
   Juu ya kazi yake
   Tusipoitenda, tutamwambiaje
   Bwana akituuliza

4. Siku ya mwisho, ndipo wataamka
   Walio mavumbini
   Ndipo wenye haki
   Watakapoimba, hosana kwa
   Bwana Yesu

97. BWANA U SEHEMU YANGU

1. Bwana U sehemu yangu
   Rafiki yangu, wewe
   Katika safari yangu
   Tatembea na wewe.

2. Mali hapa sikutaka
   Ili niheshimiwe
   Nayanikute mashaka
   Sawasawa na wewe.

3. Niongoze safarini
   Mbele unichukue
   Mlangoni pa mbinguni
   Niingie na wewe.

Pamoja na wewe
Pamoja na wewe
Katika safari yangu
Tatembea na wewe

98. MWOKOZI MOYONI MWANGU

1. Tangu siku hiyo aliponijia
   Akae moyoni mwangu
   Sina giza tena ila mwanga pia
   Kwa Yesu mwokozi wangu

   Amani moyoni mwangu
   Kwa Yesu Mwokozi wangu
   Sina shaka kamwe
   Kwa sababu Yeye
   Yu nami moyoni mwangu

2. Sina haja tena ya kutangatanga
   Ndiye kiongozi wangu
   Dhambi zangu zote zimeondolewa
   Na Yesu Mwanawe Mungu

3. Matumaini yangu ni ya hakika
   Katika Mwokozi wangu
   Hofu yangu na hamu zimeondoka
   Kwa kuwa ninaye Yesu

4. Siogopi tena nikiitwa kufa
   Yu nami daima Yesu
   Mlango wa mbinguni ni Yeye pia
   "Tapita humo kwa damu"

5. Nitaketi na Yeye huko milele
   Nisifu Mwokozi wangu
   Nina raha moyoni majira yote
   Kwa Yesu Mwanawe Mungu

99. KARIBU RAFIKI KWA YESU

1. Karibu rafiki kwa Yesu, uokolewe
   Yeye alimaliza yote msalabani

2. Ewe ndugu unaonaje? Yesu akwita
   Usiwe na moyo mgumu kumpokea

3. Sasa Baba tunakuomba utusaidie
   Twakwimbia kwa furaha ulimwenguni

Njia iko tayari leo kama wataka maisha
Ya kweli. Nawe utauona Ufalme wake.

100. NIMEKOMBOLEWA NA YESU

1. Nimekombolewa na Yesu
   Aliyenirehemia
   Kwa bei ya mauti yake
   Nimekuwa mtoto wake

   Kombolewa, kombolewa
   Nakombolewa na damu
   Kombolewa, kombolewa
   Mimi mwana wake kweli

2. Kukombolewa nafurahi
   Kupita lugha kutamka
   Kulionyesha pendo lake
   Nimekuwa mtoto wake

3. Nitamwona uzuri wake
   Mfalme wangu wa ajabu
   Na sasa najifurahisha
   Katika neema yake

4. Najua taji imewekwa
   Mbinguni tayari kwangu
   Muda kitambo atakuja
   Ili alipo niwepo

101. NJOONI TUMWABUDU MUNGU

1. Watu wote duniani, Njooni tumwabudu Mungu
   Yatupasa tukumbuke, Siku hizi ni za mwisho

   Na mimi..mimi, na wawe.. wewe
   Njoo tumwabudu Mungu

2. Yatupasa tukumbuke, Siku lle ya Bwana Yesu
   Alikufa msalabani, Akatuondolea dhambi

3. Aliwafia wenye dhambi, Wenye dhambi waokolewe
   Kwa hivyo ndugu zangu, Yatupasa tumkumbuke

4. Ndugu zangu namwambia, Mambo yale ya kweli
   Siku hiyo ya mwisho, Mtalia machozi

102. ZAENI MATUNDA

1. Zaeni matunda mema
   Zaeni matunda yale
   Zaeni yenye Baraka
   Zaeni ya heri

2. Safisha mwenendo wako
   Safisha matendo yako
   Safisha na Bwana Yesu
   Safisha yote

3. Fanyeni kazi kindugu
   Fanyeni kazi kwa bidii
   Fanyeni na Bwana Yesu
   Fanyeni yote.

4. Tolea matunda yako
   Pamoja na moyo wako
   Naye Bwana Mungu
   Wako atakubariki

5. Baraka za Mungu Baba
   Baraka za Mungu mwana
   Na za Roho Mtakatifu
   Ziwe nanyi nyote

Bwana akiyapokea
Yatabarikiwa vyema
Zaeni matunda mema
Zaeni ya heri

103. TWENDE KWA YESU

1. Twende kwa Yesu mimi nawe
   Njia atwonya tuijue
   Imo chuoni na mwenyewe
   Hapa asema, njoo

   Na furaha tutaiona
   Mioyo ikitakata sana
   Kwako Mwokozi, kuonana
   Na milele kukaa.

2. "Wana na waje" atwambia
   Furahini mkisikia
   Ndiye mfalme wetu pia
   Na tumtii, njoo!

3. Wangojeani? Leo yupo:
   Sikiza sana asemapo
   Huruma zake zikwitapo
   Ewe kijana, njoo!

104. NITAONGOZWA NA BWANA

1. Aniongoza po pote
   Nimwandame siku zote
   Kwa ajili yangu mimi
   Aliuwawa kalvari

   Nitaongozwa na Bwana, Usiku kucha na mchana
   Yesu rafiki wa heri, Ninakumbuka kalvari

2. Lanitosha neno lake
   Nishikwe na mkono wake
   Mapenzi yake ni heri
   Yalitimizwa kalvari

3. Nitaendelea mbele
   Pamoja naye milele
   Pendo lake ni hiari
   Bwana Yesu wa Kalvari

105. NILIPOTEA NA KUTANGANGA

1. Nilipotea na kutangatanga
   Mwenye bahari ya dhambini
   Bwana Yesu aliniita nyumbani
   Nikae kwake salama

   Nimo safarini nimetia nanga
   Dhambini sitarudi tena
   Hata pepo na dhoruba zikivuma
   Kwake Yesu niko salama

2. Namsifu Yesu ameniokoa
   Namwimbia kwa furaha
   Yesu pekee mwokozi wa ulimwengu
   Kimbilio, ngome, bandari

3. Ni wa salama huyu Bwana Yesu
   Tumaini la hakika
   Mikononi mwake hakuna shaka
   Kimbilio, ngome, bandari

4. Njoo kwa mwokozi anakungojea
   Akuokoe kabisa
   Kimbilia leo kituoni mwake
   Uwe wake hata milele

106. UKAE NASI

1. Mungu Baba yangu
   Nawaona watu
   Wameacha njia zako
   Na kutangatanga
2. Ukae nasi, ukae nasi
   Usiache sisi
   Ukae nasi, ukae nasi
   Tufike Mbinguni
3. Maisha yetu
   Yamepungukiwa
   Lakini tunakuamini
   Unayekaa nasi
4. Watu huzaliwa
   Na wao kukua
   Halafu mauti huja
   Mungu ukae nasi

107. BWANA MUNGU ALISEMA NA NUHU

1. Bwana Mungu alisema na Nuhu
   Akamwambia Nuhu fanyiza safina x2

   Watu walilia.. sana
   Wakaangamia... wote
   Walilia Nuhu fungua mlango
   Nuhu akajibu... sasa
   Sina la kufanya...mimi
   Bwana Mungu ameuchukua ufunguo

2. Vishike viumbe vya aina zote
   Nuhu sikia uviingize safinani x2
3. Siku ya mwisho mvua ikanyesha
   Muda wa siku arobaini duniani x2
4. Watu wote duniani walikufa
   Hata wanyama na wadudu duniani x2
5. Bwana Yesu Mwokozi alisema
   Tubuni dhambi tusiangamie na sisi x2

108. MBELE NINAENDELEA

1. Mbele ninaendelea,
   Ninazidi kutembea
   Maombi uyasikie
   Ee Bwana unipandishe

2. Sina tamani nikae
   Mahali pa shaka, kamwe
   Hapo wengi wanakaa
   Kuendelea naomba

3. Nasikia duniani
   Ni mahali pa shetani
   Natazamia mbinguni
   Nitafika na amani

4. Nataka nipandishwe juu
   Zaidi yale mawingu
   Nitaomba nifikishwe
   Ee Bwana unipandishe

Ee, Bwana, uniinue, Kwa imani nisimani
Nipande milima yote, Ee Bwana, unipandishe

109. WOTE WATANGAZIENI

1. Watu wote watangazieni, Neno la Muumba Mungu
   Wamwamini na kutubu dhambi, Watu wote watangazieni
   Neno la Muumba Mungu, Wamwamini na kutubu dhambi

   (Wambieni) watu wote, Leo na Kesho
   Wamwamini Bwana Yesu, Kweli kabisa
   (Naku) Nakushika neno lake, Bwana milele
   Na kuomba kwa Muumba wao

2. Watu wote wasiomwamini, Bwana atakaporudi
   Watachomwa na shetani wao, Watu wote wasiomwamini
   Bwana atakaporudi, Watachomwa na shetani wao

3. Watu wote watakapotenda, Dhambi za kuchokoza Mungu
   Watahukumiwa na Mwokozi wao, Watu wote watakapotenda
   Dhambi za kuchokoza Mungu, Watahukumiwa na Mwokozi wao

110. UMECHOKA UMESHUSHWA MOYO

1. Umechoka, umeshushwa moyo?
   Mwambie Yesu, mwambie Yesu,
   Una huzuni, huna furaha?
   Mwambie Yesu sasa.

   Mwambie Yesu, mwambie Yesu, Amejulika sana
   Hayuko rafiki kama Yesu, Mwambie Yesu sasa

2. Unalia juu ya haja zako?
   Mwambie Yesu, mwambie Yesu
   Mbona wazificha dhambi zako?
   Mwambie Yesu sasa

3. Waogopa? Usihuzunike
   Mwambie Yesu, mwambie Yesu;
   Una hofu kwa mambo ya mbele
   Mwambie Yesu sasa.

4. Waogopa uwazapo kifo?
   Mwambie Yesu, mwambie Yesu;
   Wautamani ufalme wake?
   Mwambie Yesu sasa.

111. LIKO LANGO MOJA WAZI

1. Liko lango moja wazi
   Ni lango Ia mbinguni
   Na wote waingiao
   Watapata nafasi

2. Yesu ndiye lango hili
   Hata sasa ni wazi
   Kwa wakubwa na wadogo
   Tajiri na maskini

3. Hili ni lango Ia raha
   Ni lango la rehema
   Kila mtu apitaye
   Hana machozi tena

4. Tukipita tango hili
   Tutatua mizigo
   Tuliochukua kwanza
   Tutavikwa uzima

5. Hima ndugu tuingie
   Lango halijafungwa
   Likifungwa mara moja
   Halitafunguliwa

Lango ndiye Yesu Bwana
Wote waingie kwake (Lango)
Lango, lango, lango, lango
La mbinguni ni wazi

112. TWENDENI ASKARI

1. Twendeni askari, watu wa Mungu
   Yesu yuko mbele, tumwandame juu
   Ametangulia Bwana vitani
   Twende mbele kwani ndiye amini

   Twende askari watu wa Mungu
   Yesu yuko mbele, tumwandame juu

2. Jeshi Ia shetani, likisikia
   Jina Ia Mwokozi, litakimbia
   Kelele za shangwe zivume nchi
   Ndugu inueni zenu sauti

3. Kweli kundi dogo, watu wa Mungu
   Sisi na mababa tu moja fungu
   Hatutengwi nao, moja imani
   Tumaini moja, na moja dini

4. Haya mbele watu nasi njiani
   Inueni mioyo, nanyi sifuni
   Heshima na sifa ni ya Mfalme
   Juu hata chini, sana zivume

113. MUNGU YUKO NASI HAPA

1. Mungu yuko nasi hapa
   Kwa Roho kutufufua
   Tazameni mawinguni
   Yako karibu kunyesha

2. Mungu yuko nasi hapa
   Mioyo yetu imemwona
   Mioyo yetu itukuzwe
   Kwa hiyo neema yako

   Tunyeshewe twakuomba
   Umande wenye Baraka
   Twangojea, twangojea
   Ufufue mioyo yetu

3. Mungu yuko nasi hapa
   Haja zetu twazileta
   Upendo wake uwashe
   Mioyo yetu iwakishwe

4. Mwokozi utusikie
   Maombi yetu tupewe
   Yafungue madirisha
   Tupate kubarikiwa

114. MUNGU AWE NANYI DAIMA

1. Mungu awe nanyi daima
   Hata twonane ya pill,
   Awachunge kwa fadhili,
   Mungu awe nanyi daima.

2. Mungu awe nanyi daima;
   Ziwafunike mbawaze,
   Awalishe, awakuze;
   Mungu awe nanyi daima.

   Hata twonane huko juu,
   Hata twonane kwake kwema;
   Hata twonane huko juu,
   Mungu awe nanyi daima.

3. Mungu awe nanyi daima;
   Kila wakati wa zani
   Awalinde hifadhini;
   Mungu awe nanyi daima

4. Mungu awe nanyi daima;
   Awabariki sana,
   Awapasulie kina;
   Mungu awe nanyi daima.

115. TEMBEA NAYE

1. Tembea naye, Tembea naye
   Tembea na Bwana Yesu

   Ingawa mchana, ingawa usiku
   Tembea na Bwana Yesu, Tembea na Bwana Yesu

2. Hata nyumbani, Tembea na Yesu tembea
   Hata nyumbani, Tembea na Yesu tembea

3. Kila mahali, Tembea na Yesu tembea
   Kila mahali , Tembea na Yesu tembea

116. KAZI YAKE BWANA YESU

1. Kazi yake Yesu ilipomalizika
   Aliwaita wanafunzi wake
   Akawaambia mambo haya yote
   Kule Gethsemane

   Yule Yuda kamwambia Wayahudi akisema
   Nitakaye mbusu ndiye huyo Mkamateni
   Mkamateni x2

2. Neno lake Yesu likawa hivi
   Hivi sasa Baba yamemalizika
   Ulivyonituma hapa duniani
   Nimeyatimiza

3. Walikwenda kule kwake Gethsemane
   Wakamwona yule Bwana Yesu
   (Yuda) Akambusu akamkumbatia
   Wakamfungafunga

4. Walimpeleka kortini mwa Kayafa
   Alihukumiwa kwenda kwa Pilato
   Alipofika kule kwa Pilato
   Pilato ni liwali

5. Walimpeleka tena kwenda kwa Pilato
   Alihukumiwa kupigwa mijiledi
   Alipokwisha kupigwa mijiledi
   Ndipo kasulubiwa

117. NJIA ILE NI NYEMBAMBA

1. Njia ile ni nyembamba iendayo uzimani
   Njia ile ni nyembamba iendayo uzimani

2. Na wamama wanaweza kuiona njia hiyo
   Njia hiyo ni nyembamba iendayo uzimani

3. Na vijana wanaweza kuiona njia hiyo
   Njia hiyo ni nyembamba iendayo uzimani

4. Na wazee wanaweza kuiona njia hiyo
   Njia hiyo ni nyembaba iendayo uzimani

118. YESU, YESU AMEFUFUKA

1. (Yesu, Yesu) amefufuka, amefufuka
   Ameshinda dhambi na mauti, amefufuka
   (Akina baba tumwendee) amefufuka
   (Na sisi sote tumwendee) amefufuka
   (Yesu, Yesu) amefufuka
   Ameshinda dhambi na mauti, amefufuka
2. (Yesu, Yesu) umefufuka, umefufuka
   Ushindi wako huokoa, Wewe Mwokozi
   (Ujifunue na kwetu) Mwokozi wetu
   (Utupe wokovu wako) Mwokozi wetu
   (Twakuamini, ee Bwana) Mwokozi wetu
   (Yesu, Yesu) umefufuka
   Ushindi wako huokoa, wewe Mwokozi
3. (Yesu, Yesu) umefufuka, Umefufuka
   Sisi sote utatufufua siku ya mwisho
   (Twakungojea kwa shangwe) Yesu Mfalme
   (Fahari yako tuone) Yesu Mfalme
   (Yesu, Yesu) umefufuka
   Sisi sote utatufufua siku ya mwisho

119. MZIGO WA DHAMBI

1. Mzigo wa dhambi hauwezi kuingia x2
   Kweli hauwezi kuingia x2
2. Ukiwa mlevi hauwezi kuingia x2
   Kweli hauwezi kuingia x2
3. Ukiwa na chuki hauwezi kuingia x2
   Kweli hauwezi kuingia x2
4. Ukiwa mwongo hauwezi kuingia x2
   Kweli hauwezi kuingia x2
5. Ukiwa na Yesu utaweza kuingia x2
   Kweli utaweza kuingia x2

120. MKARIBISHE YESU

1. Mkaribishe rafiki, Mkaribishe mkaribishe
   Anakuja kwako sasa, Mkaribishe
2. Ni rafiki wako sasa, Mkaribishe mkaribishe
   Anakuja kwako sasa, Mkaribishe
3. Yesu ni rafiki wako, Mkaribishe mkaribishe
   Anakuja kwako sasa, Mkaribishe
4. Kwa yeye utaokoka, Mkaribishe mkaribishe
   Anakuja kwako sasa, Mkaribishe
5. Sikia sauti yake, Mkaribishe mkaribishe
   Anakuja kwako sasa, Mkaribishe

121. TUNAYO SAFARI

1. Tunayo safari ya kwenda
   Mbinguni, mbinguni kwa Baba
   Tunayo safari ya kwenda
   Mbinguni, mbinguni, kwa Baba

   (Njiani) Kuna vikwazo vinavyokwaza watu
   (Visiki) Na makonge ya kuangusha wengi
   (Ni nani) Awezaye kutuondolea yote
   (Hakuna) Mwingine ila Yesu Mwokozi

2. Safari ni ndefu ya kwenda
   Mbinguni, na tena ni ngumu
   Safari ni ndefu ya kwenda
   Mbinguni, tena ni ngumu
3. Ulevi, uzinzi, uongo na chuki
   Visiki na makonge njiani
   Ulevi, uzinzi uongo na chuki
   Visiki na makonge njiani
4. Visiki ni dhambi makonge ni
   Dhambi tujihadhari zote.
   Visiki ni dhambi makonge ni
   Dhambi, tujihadhari zote.

122. YESU KWA IMANI

1. Yesu kwa imani
   Nakutumaini
   Peke yako
   Nisikie sasa
   Na kunitakasa
   Ni wako kabisa
   Tangu leo

2. Nipe nguvu pia
   Za kusaidia
   Moyo wangu
   Ulikufa Wewe
   Wokovu nipewe
   Nakupenda Wewe
   Bwana wangu

3. Hapa nazunguka
   Katika mashaka
   Na matata;
   Palipo na giza
   Utaniongoza
   Hivi nitaweza
   Kufuata

4. Takuwa mzima
   Nivushe salama
   Mautini
   Sina hofu kamwe
   Ukiwapo name
   Nami nikwandame
   Utaniongoza, Siku zote

123. ALIGUSA UPINDO WA NGUO

1. Aligusa upindo wa nguo
   Mara akaona amepona
   Hivi sasa ni saa ya kujua
   Neno lake imara

2. Akaenda akitetemeka
   Akasikia uwezo wake
   Akasema Bwana Yesu wangu
   Mungu na asifiwe

3. Njoo tumfukuze Shetani
   Bwana Yesu ndiye kiongozi
   Vita vikali tuvishinde
   Mungu na asifiwe

4. Njoo sasa tusiwe na hofu
   Bwana Yesu ndiye kiongozi
   Vita havitakushinda wewe
   Mungu na asifiwe.

Bwana Yesu akuita njoo njoo
Bwana Yesu akuambia rudi rudi
Mtazame Bwana Yesu juu juu, Dhambi zitasafishwa
Yii yiyi yiii Haha haha haaaa
Mtazame Bwana Yesu juu juu
Dhambi zitasafishwa

124. JIWE KUU LA PEMBBENI

1. Mungu ni Baba wetu
   Ndiye Muumba wa vyote
   Uwezo na ushindi
   Hupatikana kwake

2. Bwana wetu ni Kristo
   Ndiye mwamba wa pekee
   Jiwe kuu la pembeni
   Liliwekwa na Mungu

3. Yesu alilijenga
   Kanisa juu ya mwamba
   Milango ya kuzimu
   Haiwezi kushinda

4. Naye Yesu ni kichwa
   Ni kichwa cha kanisa
   Naye ni mzaliwa
   Wa kwanza toka wafu

5. Mungu Baba atukuzwe
   Baba na Bwana Yesu
   Aliyetubariki
   Baraka za rohoni

Bwana Mungu asema
Tazama naliweka
Jiwe kuu la pembeni
Lililo jaribiwa

125. TUBU DHAMBI

1. Bwana Yesu alipita mji wa Yeriko
   Alimwona Batimayo naye ni Kipofu
   Bwana Yesu alipita Mji wa Yeriko
   Alimwona Batimayo naye ni Kipofu

   Kwa nini?...Ewe ndugu
   Kwa nini?...Hujatubu dhambi
   Kwa nini?...Ewe ndugu kweli
   Tubu dhambi zako.x2

2. Zamani za kale nilikuwa mwenye dhambi
   Bwana Yesu alikuta nikitangatanga
   Zamani za kale nilikuwa mwenye dhambi
   Bwana Yesu alikuta nikitangatanga

3. Mwito wa huruma kweli ndugu yangu
   Usikawie kufika, Yesu akuita
   Mwito wa huruma kweli ndugu yangu
   Usikawie kufika, Yesu akuita

126. KUTIMIZA AHADI

1. Utukufu ulionipa Baba
   Nimewapa hawa ulionipa
   Utukufu ulionipa Baba
   Nimewapa hawa ulionipa

   Ili wawe na umoja na Baba
   (Ewe Baba)
   Kama sisi tulivyo na umoja
   (Ewe Baba)
   Nataka nilipo nao wawepo
   (Mungu wangu)
   Wautazame utukufu wangu x2

2. Kuna watu ninaowaombea
   Na wengine wanaoniamini
   Kuna watu ninaowaombea
   Na wengine wanaoniamini

127. NDUGU WA KOROHONI

1. Ndugu wa kirohoni
   Mliokombolewa
   Tafakarini sana
   Yatupasayo

2. Siku itatimia
   Tutakapoulizwa
   Wale wa nyumba zetu
   Na majirani

3. Tujitoeni ndugu
   Tukahubiri Injili
   Atutumie Roho
   Kuponya wengi

4. Wasiokombolewa
   Ni wengi vijijini
   Wataokolewa je
   Tukiogopa?

5. Bwana alijitoa
   Akapotewa mengi
   Ili atuokoe
   Tusiwa waoga

Wapenzi wake Yesu
Tuliokombolewa
tujitoe kabisa
Wengi waponye

128. BWANA AMEFUFUKA

1. Bwana amefufuka, Aleluya.
   Twimbe na malaika, Aleluya.
   Sifa zetu na shangwe Aleluya.
   Na zao zisitengwe Aleluya.

2. Ukombozi timamu, Aleluya.
   Umetimu kwa damu, Aleluya
   Mshindi asifiwe, Aleluya.
   Yu hai kwa milele, Aleluya.

3. Jiwe, lindo, muhuri Aleluya.
   Vi wapi? na kaburi? Aleluya.
   Kifo hakimuweki, Aleluya.
   Ametoka peponi, Aleluya.

4. Yu hai Mtukufu; Aleluya.
   Cha kifo hatuhofu! Aleluya
   Alitufia sisi, Aleluya
   Tupate kuwa huru. Aleluya.

129. NI SALAMA ROHONI MWANGU

1. Nionapo amani kama shwari
   Au nionapo shida;
   Kwa hali zote umenijulisha
   Ni salama rohoni mwangu

   Salama rohoni , Ni salama rohoni mwangu

2. Ingawa shetani atanitesa
   Nitajipa moyo kwani
   Kristo ameona unyonge wangu
   Amekufa kwa roho yangu

3. Dhambi zangu zote, wala si nusu
   Zimewekwa Msalabani
   Wala sichukui Iaana yake
   Ni salama rohoni mwangu

4. Ee Bwana himiza siku ya kuja
   Panda itakapolia;
   Utakaposhuka sitaogopa
   Ni salama rohoni mwangu

130. HAMWENDI MBINGUNI

1. Tuko safarini kwenda juu mbinguni
   Makao ya wenye furaha upendo
   Ninyi mtangao mjipotezao
   Semeni hamwendi kule juu mbinguni

   Hamwendi mbinguni? Semeni hamwendi
   Hamwendi mbinguni? Kule juu mbinguni

2. Kwenye nchi hiyo wako watukufu
   Hawana uchungu wala maumivu
   Mliolemewa mizigo mizito
   Semeni hamwendi kule juu mbinguni

3. Mbele ya kuitwa wale takatifu
   Huwa na makao yatengeneayo
   Milango minara hung'arishwa sana
   Semeni hamwendi kule juu mbinguni

4. Mbele askari! Mbingu ni yenu
   Punde mtaonja utamu wa kule
   Kitambo kidogo tutakusanyika
   Kwenye utukufu tukaburundike

131. MSIJIFADHAISHE MIOYONI

1. Ndugu msijifadhaishe mioyo
   Mwamini Mungu Baba nami niaminini x2

   Nyumba ya Baba ina makao
   Mengi nami singewambia
   Kuwaandaa (makao) na sisi zote
   Tuishi nitarudi niwachukue.

2. Huko niendako mnakujua
   Hata ile njia ya kupitia mnaijua x2

3. Mimi ndimi njia na kweli na uzima
   Mtu hafiki kwa Baba yangu pasipo mimi x2

132. PELEKA JINA LA YESU

1. Peleka jina la Yesu, Ko kote uendako
   Litafurahisha moyo, Peleka uendako

   Dhamani, na damu
   Ni jina lake Yesu
   Dhamini, na damu
   Ni jina lake Yesu

2. Peleka jina la Yesu, Liwe silaha zako
   Utakapojaribiwa, Lilia jina hilo

3. Yesu, jina la dhamani, Limenifurahisha
   Nikiwasili mbinguni, Atanikaribisha

4. Kwa jina la Bwana Yesu, Nimejiinamisha
   Ndiye mfalme wa wafalme, Katika ya maisha

133. WAMWENDEA YESU KWA KUSAFIWA

1. Wamwendea Yesu kwa kusafiwa
   Na kuoshwa kwa damu ya kondoo?
   Je neema yake umemwagiwa
   Umeoshwa kwa damu ya kondoo?

   Kuoshwa, kwa damu
   ltutakasayo ya kondoo
   Ziwe safe nguo nyeupe mno
   Umeoshwa kwa damu ya kondoo?

2. Wamwandama daima mkombozi
   Na kuoshwa kwa damu ya kondoo?
   Je neema yake umemwagiwa
   Umeoshwa kwa damu ya kondoo?

3. Atakaporudi Bwana – arusi
   Uwe safi kwa damu ya kondoo!
   Yafae kwenda Mbinguni mavazi
   Umeoshwa kwa damu ya kondoo

4. Yatupwe yalipo na takataka
   Na uoshwe kwa damu ya kondoo
   Huoni kijito cha tiririka
   Na uoshwe kwa damu ya kondoo

134. DENI YANGU YA DHAMBI

1. Deni yangu ya dhambi
   Yesu amelipa
   Kwake msalabani
   Nilipewa uzima

2. Bwana Yesu asema
   Mwanangu dhaifu
   Uwezo na ushindi
   Hupatikana kwangu

   Deni ya dhambi
   Msatabani
   llimalizikia
   Ni huru kabisa

3. Bwana, kweli naona
   Nguvu zako pekee
   Huondoa ukoma
   Niwe kipya kiumbe

4. Sina wema moyoni
   Nidai Neema
   Nakubali kabisa
   Kwa damu kusafiwa

135. YESU ASEMA NA SISI KWELI

1. Yesu asema na sisi kweli
   MIe chuoni mwangu
   Ni kweli mimi ni mzabibu
   Na ninyi ni matawi

   Bwana atalikata
   Tawi lisilozaa
   Bwana atalitia
   Tawi hilo motoni

2. Na kama vile ninyi wanadamu
   Mkatavyo matawi
   Yasiozaa na kuyatupa
   Na vivyo Baba yangu

3. Yesu ni mwokozi wangu kweli
   Nami sina mwengine
   Yeye ni wangu, ni wangu kweli
   Na yeye ni wa kweli

136. NIKITAFAKARI UPENDO

1. Nikitafakari upendo wa Yesu
   Duniani sitarudi tena x2

   Oh! Bwana Yesu uniongoze
   Duniani kuna majaribu tele x2

2. Nilipokufuata Bwana Yesu
   Ulimwengu ulinidharau sana x2

3. Sitaona haya kukuimbia
   Ingawa adui ananizunguka x2

137. NI MWOKOZI ALIYENIFIA

1. Ni Mwokozi aliyenifia, Nitoke dhambini alisema
   "Yeye aliyemwamini Mwana, Anao uzima

   Amini, amini nakuambia
   Amini amini ujumbe mpya
   Yeye aliyemwamini Mwana, Anao uzima

2. Dhambi zangu zilichukuliwa, Deni zangu zote zililipwa
   Wote waliomwamini Mwana, Wanao uzima

3. Ijapo ningekuwa maskini, Ijapo ningekuwa mkosaji
   Neno la furaha la Mwokozi, Ninao uzima

4. Na sina shaka, nitamwamini, Yeye ajaye kwake hatupwi
   Amwaminiye, tuma habari, Tunao uzima.

138. MTETEENI YESU

1. Mteteeni Yesu, Mlio askari, Inueni beramu, Mkae tayari
   Kwenda naye vitani, Sisi hatuchoki, Hata washindwe pia
   Yeye amiliki
2. Mteteeni Yesu , Vita ni vikali, Leo siku ya Bwana
   Atashinda kweli, Waume twende naye, Adui ni wengi
   Lakini kwake Bwana, Tuna nguvu nyingi
3. Mteteeni Yesu, Wenye ushujaa, Nguvu zenu za mwili
   Hazitatufaa, Silaha ya Injili , Vaeni daima
   Kesheni mkiomba, sirudini nyuma
4. Mteteeni Yesu, Vita ni vikali, Wengi wamdharau
   Hawamkubali, Ila atamiliki, Tusitie shaka, Kuwa naye vitani
   Twashinda hakika

139. HURUMA YA BABA

1. Mwana alimwambia baba
   Baba nataka sehemu yangu x2

   Rudi Rudi Mwanangu rudi
   Rudi Rudi nitakupokea x2

2. Mwana alipopata sehemu yake
   Alihamia mbali x2
3. Mwana alipotapanya mali yake
   Akarudi kwa Baba x2
4. Baba alimhurumia mwana
   Aliporudi kwa baba

140. SIKU KARIBU KWISHA

1. Siku karibu kwisha, Ya Roho kutafuta
   Nayo siku ifike, Ya shaka na machozi

   Nachunguliya mwokozi
   Mwenye kupima mioyo
   Ya Roho Mtakatifu
   Roho karibu kwenda

2. Roho Ina machozi, Yakulilia mioyo
   Isiyoaminika, Roho karibu kwenda

3. Siku zile za mwisho, Ndizo tulizo nazo
   Mwenye akili ajue, Roho karibu kwenda

4. Dalili zimefika, Twangojea mwokozi
   Tarumbeta Italia, Roho karibu kwenda

141. HUKUMU NA MAJUTO

1. Hukumu yaningoja nitakimbilia wapi
   Ili niponywe na Bwana Yesu aita
   Hukumu yaningoja nitakimbilia wapi
   Ili niponywe na Bwana Yesu aita

   Nitasema nini Bwana?
   Dhambi zangu zanilemea
   Nitajibu nini Bwana?
   Dhambi zangu zanilemea x2

   Bwana niende wapi hukumu hii tayari
   Bwana dhambi zangu zanilemea
   Bwana niende wapi hukumu hii
   Tayari Bwana dhambi zangu zanilemea

2. Yesu alimwaga damu kutuponya sisi
   Wakosaji ili tusafishwe hima
   Yesu alimwaga damu kutuponya sisi
   Wakosaji Ili tusafishwe hima

3. Sote tumwendee mponya ni Yesu kwa nguvu
   Tumwombe kwani atatusafisha
   Sote tumwendee mponya ni Yesu kwa nguvu
   Tumwombe kwani atatusafisha

142 BABA, MWANA ROHO

1. Baba, Mwana. Roho, Mungu Mwenye enzi
   Kila tukiamka tunakuabudu
   Baba, Mwana, Roho, Mungu wa mapenzi
   Ewe Utatu, tunakusifu

2. Baba, Mwana, Roho wakuaminio
   Wanakutolea shukurani zao
   Wakusujudia malaika nao
   Wewe U mwanzo, nawe U mwisho

3. Baba, Mwana, Roho sisi tu gizani
   Utukufu wako hauoni kosa
   U Mtakatifu, nawe U mapenzi
   U peke yako, mwenzio huna

4. Baba, Mwana, Roho, Mungu Mwenye enzi
   Ulivyoviumba vyote vyakusifu
   Baba, Mwana, Roho, Mungu wa mapenzi
   Ewe utatu, tunakusifu

143. YESU KWETU NI RAFIKI

1. Yesu kwetu ni rafiki, Hwambia haja pia,
   Tukiomba kwa Babaye, Maombi asikia;
   Lakini twajikosesha, Twajitweka vibaya
   Kwamba tulimwaomba Mungu, Dua atasikia

2. Una dhiki na maonjo? Una mashaka pia?
   Haifai kufa moyo, Dua atasikia
   Hakuna mwingine mwema, Wa kutuhurumia;
   Atujua tu dhaifu, Maombi asikia

3. Je, hunayo hata nguvu, Huwezi kwendelea,
   Ujapodharauliwa, Ujaporushwa pia
   Watu wangekudharau, Wapendao dunia,
   Hukwambata mikononi, Dua atasikia

144. NITWAE HIVI NILIVYO

1. Hivi nilivyo kipofu
   Maskini na mpungufu
   Wewe umtimilifu
   Bwana Yesu naja, naja

   Nawe hivi utanitwaa, Nisidhubutu kukawa
   Na wewe hutanikataa, Bwana Yesu naja, naja

2. Hivi nilivyo mapenzi
   Yamenipa njia wazi
   Hali na mali sisazi
   Bwana Yesu, naja, naja

3. Nitwae hivi nilivyo
   Umemwaga damu yako
   Nawe ulivyoniita
   Bwana Yesu naja, naja

4. Hivyo nilivyo si langu
   Kujiosha roho yangu
   Nisamehe dhambi zangu
   Bwana Yesu naja, naja

5. Hivi nilivyo sioni
   Kamwe furaha moyoni
   Daima ni mashakani
   Bwana Yesu naja, naja

145. CHA KUTUMAINI SINA

1. Cha kutumaini sina, Ila damu yake Bwana
   Sina wema wa kutosha , Dhambi zangu kuziosha

   Kwake Yesu na simama
   Ndiye Mwamba ni salama
   Ndiye Mwamba ni salama

2. Njia yangu iwe ndefu, Yeye hunipa wokovu
   Mawimbi yakinipiga, Nguvu zake ndiye nanga

3. Damu yake na sadaka, Nategemea daima
   Yote chini yakiisha, Mwokozi ataniosha

4. Nikiitwa hukumuni, Rohoni nina Amani
   Nikivikwa taji yake, Sina hofu mbele zake

146. YESU KURUDI MBINGUNI

1. Yesu aliwaambia wanafunzi akisema
   Bado muda mchache nakwenda
   Nakwenda kwa Baba x2

   Nyumbani - mwa Baba, Mna makao, mna makao
   Mkijitahidi kuomba, (Nafasi haingalikuwako)
   Ningallwaambia, Alelluya - leo naenda
   Kwenda mimi, kwenda mimi, Ku-anda-lia
   Kisha nitarudi na ninyi, Kwa Baba

2. Msifadhaike mioyoni mwenu
   Amini Mungu Baba, amini
   Amini na mimi x2

3. Tomaso akamwambia, Bwana
   Sisi hatujui
   Uendako Baba, twajua je?
   Twajua je njia x2

4. Yesu akamjibu, mimi ndimi
   Njia na ukweli na uzima
   Mtu haji kwa Baba ila njia
   Ya mimi x2

147. BWANA YESU ANAITA

1. Bwana Yesu anaita
   Furaha za dunia acha
   Maisha haya yapita
   Usingizi amka

   Anakuita, uje leo
   Usichelewe, Leo uje kwa Yesu

2. Bwana Yesu anaita
   Tendo lake usidharau
   Kwani kungojea tena
   Akuita uje leo

3. Bwana Yesu anaita
   Kwani kuishi kifungoni
   Usiteseke dhambini
   Uhuru kwake utapata

4. Bwana Yesu anaita
   Rohoni yangu namtolea
   Sasa dunia kwa heri
   Kwa kuwa Yesu ametosha

FAHARASA

AKIITA NITAITIKA ----------29
ALIGUSA UPINDO WA NGUO ----------123
AMANI NAIWEKA ----------31
AMENIITA MWOKOZI ----------37
ANGALIA BWANA YESU ----------24
ANISIKIAYE ALIYE YOTE ----------17
ASALI YA NYUKI ----------93
ATAKUJA, ATAKUJA ----------95
AWAYE YEYOTE ----------42
BABA MUNGU NAKUSHUKURU ----------32
BABA YETU ALIYE MBINGUNI ----------35
BARAGUMU YAKE BWANA ----------28
BWANA AMEFUFUKA ----------128
BWANA AMENITUMA ---------- 4
BWANA MUNGU ALISEMA NA NUHU ----------107
BWANA MUNGU MTAKATIFU ----------47
BWANA MUNGU NA SHANGAA ----------57
BWANA U SEHEMU YANGU ----------97
BWANA YESU ANAITA ---------- 147
BWANA, MWANA, ROHO ----------142
CHA KUTUMAINI SINA ----------145
CHOMBO CHAKO ----------34
DAMU IMEBUBUNJIKA ----------26
DAMU YA YESU ----------54
DENI YANGU YA DHAMBI ----------134
ENEZA HABARI ----------56
FURAHA KWA ULIMWENGU ---------- 69

HAKUNA RAFIKI ----------65
HAMWENDI MBINGUNI ----------130
HARUSI TAKATIFU ----------87
HUKUMU INAKUJA ----------45
HUKUMU NA MAJUTO ----------141
HURUMA YA BABA ----------139
JINA LA YESU ----------2
JINA LAKE IMANUELI ----------84
JIWE KUU ----------124
KARIBU NAWE, EE MWOKOZI ----------59
KARIBU RAFIKI ----------99
KATIKA MJI WA TARSO ----------6
KAZI YAKE BWANA YESU ----------116
KAZI YANGU IKIISHA ----------50
KUMTEGEMEA MWOKOZI ----------67
KUPIGANA VITA ----------39
KUTIMIZA AHADI ----------126
KWA KALVARI ----------40
LIKO LANGO MOJA WAZI ----------111
MATAIFA WATAKUSANYA ----------81
MBELE NINAENDELEA ----------108
MEZA YA BWANA ----------53
MILIMA NA MABONDE ----------83
MIMI NDIYE WA KWANZA ----------68
MJI MZURI ----------36
MJI WA YERUSALEMU ----------64
MKARIBISHE YESU ----------120
MLE KABURINI ----------41
MSIJIFADHAISHE MIOYONI ----------131

MTETEENI YESU ----------138
MUNGU AWE NANYI DAIMA ----------114
MUNGU MTUKUFU ALIYE BWANA ----------15
MUNGU NI PENDO ----------77
MUNGU YUKO NASI HAPA ----------113
MWAMBA WENYE IMARA ----------25
MWAMINI YESU ----------74
MWANANGU KARIBU ----------16
MWOKOZI MOYONI MWANGU ----------98
MWOKOZI WETU NI MWAMBA ----------82
MZIGO WA DHAMBI ----------119
NAENDEA MSALABA ----------66
NAMDHANIA YESU MWOKOZI ----------7
NASIKITIKA SANA ----------33
NDIYO DHAMANA YESU WANGU ----------51
NDUGU WA KIROHONI ----------127
NI MWOKOZI ALIYENIFIA ----------137
NI SALAMA ROHONI ----------129
NI SIKU KUU ----------92
NI TABIBU WA KARIBU ----------23
NIKITAFAKARI UPENDO ----------136
NILIPOTEA NA KUTANGATANGA ----------105
NIMECHOKA NAZO DHAMBI ----------94
NIMEKOMBOLEWA ----------100
NIMEKUBALI KUMFUATA YESU ----------21
NIMELEMEWA NA HATIA ZANGU ----------76
NIMEPATA NJIA ----------55
NINA HAJA NAWE ----------43
NIONAPO MTI BORA ---------- 58

NIONGOZE, BWANA YESU ----------75
NITAKUWA WAPI YESU AKIJA ----------96
NITAONGOZWA NA BWANA ----------104
NITWAE HIVI NILIVYO ----------144
NJIA ILE NYEMBAMBA ----------117
NJONI NA FURAHA ----------38
NJOONI TUMWABUDU MUNGU ----------101
NYUMBA YA BABA ----------79
OMBI ----------19
PANDA ASUBUHI ----------60
PELEKA JINA LA YESU ----------132
PELELEZA NDANI YANGU ----------12
SAFARI YA KUNGOJA ----------10
SASA NDIO WAKATI ----------89
SHANGILIA ----------9
SI DAMU YA NYAMA ----------91
SIKU KARIBU KWISHA ----------140
SIKU ZA MWISHO ---------- 5
SIMAMA IMARA ----------48
SIONI HAYA KWA BWANA ----------20
SIOSHWI DHAMBI ZANGU ----------85
SITAONA GIZA YESU AJAPO ----------30
TANGAZA M I LI MAN I ----------52
TARUMBETA YAKE BWANA ----------13
TAZAMA KULE KALVARI ----------14
TEMBEA NAYE ----------115
TOKA UTUMWANI ----------73
TUBU DHAMBI ----------125
TUMESAFISHWA ----------44

TUNAOMBA ROHO ----------18
TUNAYO SAFARI ----------121
TWAMSIFU MUNGU ----------88
TWENDE KWA YESU ----------103
TWENDE KWAKE ---------- 72
TWENDENI ASKARI ----------112
TWONANE MILELE ----------62
UKAE NASI ----------106
UMECHOKA UMESHUSHWA MOYO ----------110
UMOJA ----------1
UPENDO ----------3
USIKU MKUU ----------46
USINIPITE MWOKOZI ----------61
WACHUNGA WALIPOLINDA ----------78
WAIMBA SIKIZI ----------70
WAISRAELI KUTOKA MISRI ----------80
WAMWENDEA YESU ----------133
WANDUGU NA WADADA ----------49
WOTE WATANGAZIENI ----------109
YESU AKIJA TUTAFANYA NINI ----------22
YESU ALIKUFA ----------11
YESU ASEMA NA SISI KWELI ----------135
YESU ATAKA KIANGA ----------71
YESU KURUDI MBINGUNI ----------146
YESU KWA IMANI ----------122
YESU KWETU NI RAFIKI ----------143
YESU MPONYA ----------63
YESU MSALABANI ----------86
YESU NDIYE MZABIBU ----------8

YESU NI JINA NIPENDALO ----------27
YESU, YESU AMEFUFUKA ----------118
YOTE NAMTOLEA YESU ----------90
ZAENI MATUNDA ----------102

INAKUPASA KUJUA NJIA YA KWELI UINGIE KATIKA KANISA

KUMWAMINI KRISTO: Yohana 8:24, Matendo 16:31, Waebrania 11:6

NI LAZIMA. KUZITUBIA DHAMBI: Luka 13:3, Matendo 2:38, 3:19, 17:30

KUKIRI IMANI YAKO KATIKA YESU: Mathayo 10:32-33, Warumi 10:10, Matendo 8:36-37

NI LAZIMA KUBATIZWA: Mathayo 28:19, Marko 16:16, Matendo 2:38, 10:48, 22:16, I Petro 3:21

KANISA

Kanisa alilolijenga Yesu si jengo. Yesu alipopanga Kanisa lake, hakutaka kanisa lililojengwa na mawe wala mbao kama ile hekalu la kale huko Yerusalemu. Hekalu zilizojengwa na huharibika au kuangamizwa ijapokuwa zilijengwa na mawe mazuri mno. Kanisa la Yesu limejengwa mioyo na roho ya watu. Biblia inataja kitu cha kujenga kanisa, "MAWE YALIYO HAI" *(I Petro 2:5; 1 Wakorintho 6:19).* Kanisa la Yesu ni watu. Kanisa la Kristo halifungwi mahali pamoja kama jengo la mawe, bali Kanisa hudumu po pote palipo wanaume au wanawake waaminio. Kanisa ni baraka kuu kutoka kwa Mungu. Pengine Shetani amejishughulisha sana kwa miaka mingi kuliharibu kanisa kwa sababu amelitambua kuwa baraka kuu ya Mungu. Siku hizi, kanisa la Kristo peke yake hufuata kielelezo cha Mungu kwa ajili ya kanisa kinachopatikana katika Biblia. Baada ya siku za mitume lile kosa la kwanza lililoingia kanisani lilikuwa kubadilisha uongozi wake. Watu wengine wanaotaka kwa ukosefu wa dini na kuingia kanisa la Agano Jipya washangaa sana kwa sababu ya urahisi wa uongozi wake. Uongozi huo si kama madhehebu yanayo mambo mengi ndani ya uongozi wao. Sasa tusome kielelezo rahisi cha Mungu kuhusu uongozi wa kanisa lake.

YESU Ndiye Kichwa

Haiwezekani serekali, chama, au kundi kudumu pasipo na kichwa. Uongozi wa kundi ni wajibu wa kichwa. Huo ni utaratibu wa dunia, tena utaratibu wa kanisa. Mungu alimweka Yesu kuwa kichwa cha pekee kwa kanisa. *Waefeso 1:22-23* inasema kwamba Mungu "alimweka Yesu awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa ambalo ndilo mwili wake." Kama mume ni kichwa juu ya jamii, vile Yesu ni kichwa juu ya kanisa *Waefeso 5:23; Wakolosai 1:18.* Mungu hakubali kichwa kingine kwa kanisa ila Yesu tu. Wakristo wa kweli, walipo pote, ni "mwili" wa Yesu Kristo. Hawafuati kichwa kingine.

Haiwezekani mtu awe Kichwa cha Kanisa

Kanisa lo lote ambalo mwanadamu ndiye kichwa, mwenye kiti, au kiongozi mkuu si kanisa la kweli la Biblia. Soma *Mathayo 28:18- 19.* Hapo Yesu aeleza kwamba amepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Yeye ni kiongozi wa pekee wa kiroho kustahili atuongoze kufika kwa Baba. Hakuna mamlaka mwanadamu achukue ukuu wa Yesu aliopewa na Mungu. Mwanadamu kuwa kichwa cha kanisa ni dhambi.

UTARATIBU

Kanisa ni la Mungu--si La wanadamu. Mungu amepanga utaratibu wa kanisa. Kwa hivyo, watu hawawezi kutunga utaratibu ili wapendezwe. Biblia hutoa wazi mipango ya Mungu inayohusu kanisa. Mwanadamu hana haki ya kubadilisha mpango huo.

Wazee

Ni mapenzi yake Mungu kwamba kazi na ibada ya kila kundi la kanisa iwe chini ya waangalizi na wazee. Wazee huongoza kanisa wakitimiza amri na mafundisho ya Yesu. Wazee sio wenye kutawala kanisani. Wazee ni mifano ya wema kwa ajili ya kanisa. Wanapasa kuangalia mambo ya uzima wa kiroho kwa ajili ya kila Mkristo.

Katika *Matendo 20:17-28* twasoma kwamba Mtume Paulo alitumia majina mengine mawili ile "Wazee" kwa kutaja viongozi wa kundi la kanisa. Majina hayo ni maaskofu (waangalizi) na wachungaji *(mst. 28).* "Muchungaji" maana yake ni pastor. Soma *Tito 1:5-7.* Hapo, tena, Biblia huonyesha kwamba "mzee" na "askofu" ni sawa. Majina haya: mzee, askofu, pastor, mwangalizi na mchungaji, yote yatajwa kuhusu jamii moja ya watu.

Agano Jipya huonyesha kwamba ni lazima kila kundi live na wazee zaidi ya mmoja. Tena, hakuna wazee wenye amri ya kutumikia zaidi ya kanisa moja Kila kanisa linapaswa kuwa na wazee wake lenyewe.

Siyo watu wote wanoweza kuchaguliwa wazee. Mungu ametaja tabia fulani ya wazee wanoongoza kanisa. Orodha za tabia hizi zimepatikana katika *I Timotheo 3:1-7 na Tito 1:5-9.* Soma mistari hiyo kwa uangalifu.

MASHEMASI

"Shernase maana yake ni mtumishi. Watumishi waliochaguliwa na kanisa katika *Matendo 6:1-6* walifanya kazi ya kanisa ili shida za kanisa zisizuie maendeleo ya Injili. Waliwalisha wenye njaa ili mitume waweze kuhubiri na kuomba daima. Mfano huo hutuonyesha kwamba kazi ya mashemasi ni muhimu sana katika kanisa.

Kama vile wazee wa kanisa inawapasa mashemasi watimize tabia fulani. Watu wema, tu, waliojaa na Roho na hekima waweza kushika kazi hiyo *(Matendo 6:3).* Tabia ya mashemasi imepatikana katika *I Timotheo 3:8-13.* Soma orodha hiyo kwa uangalifu.

Wainjilisti

Mawazo ya watu wengi kuhusu kazi mwinjilisti au mhubiri yafuatana na mapokeao yao badala ya kufuatana na Agano Jipya. Na makosa mengi hutokana na mawazo

hayo. Mhubiri si Mwangalizi wala mchungaji wa kanisa. Kazi ya kuangalia na kuchunga kanisa ni kazi ya wazee. Vile vile, mhubiri si kichwa cha pekee katika kanisa. Mhubiri asiitwe "mchungaji" wala "pastor." Sababu wazee ni wachungaji *(Matendo 20:28)*

Yafuatayo ni mafundisho ya Biblia juu ya kazi ya mwinjilisti:

1. Ahubiri neno (2 Tirnotheo 4:2-5).
2. Alete habari njema kwa ulimwengu ambao umepotea. Aokoe roho za watu (*2 Wakorintho 5:18-20).*
3. Hujenga kanisa (Waefeso 4:11-16).
4. Awasaidie waume wazidi kiroho ni wafikie kuwa wazee na mashemasi. Awasaidie wake wawe bibi wema wa bwana na mama wema wa watoto *(Tito 1:5).*
5. Akinge imani wakati wa mashambulio ya Shetani *(1 Timotheo 1:3; Tito 1:10-13).*
6. Afundishe wengine wafike kuwa wahubiri *(2 Timotheo 2:2).*

Wakristo Wote

Si Wakristo wote wawezao kufanya kazi ya wahubiri. wazee, au mashemasi. Walakini Biblia yasema kwamba Wakristo wote ni makuhani *(1 Petro 2:9).* Yesu ni Kuhani Mkuu. Wakristo wote hushiriki ukuhani *(Waebrania 7:21- 8:2).* Ni Kosa kufundisha kwamba Wakristo wachache maalum ni makuhani ya kanisa.

Kama makuhani, Wakristo wote hustahili kuzungumza na Mungu kwa njia ya Yesu, kuhani Mkuu. Wakristo wote wastahili pia kusoma na kufahamu Biblia pasipo hofu. Kwa Kuwa ni makuhani, Wakristo wote ni wenye wajibu wa kuwa waaminifu na kumtii Mungu katika yote wamepewa kazi ya kuokoa roho za watu kwa ajili ya Yesu.

Kujitawala kwa Kanisa

Tukisoma kwa uangalifu *Matendo 20:17-28 na 1 Petro 5:1-3,* tutafahamu kwamba inawapasa wazee wa kanisa waongoze kundi moja, tu. Siyo mapenzi ya Mungu wawe maaskofu au waangalizi juu ya makanisa mengi. Mungu kwa hekima yake ameliacha kila kundi huru ili lijitawale chini ya Bwana Yesu. Kuna faida kubwa katika utaratibu huo. Kundi moja likipunguka katika imani, haliwezi kuingiza mengine katika kosa lake. Umoja wa kweli hutokana kwa Mungu na ni umoja wa imani na kutii kwa neno la Mungu

IBADA

Soma kwa uangalifu *Yohana 4:12-23.* Mistari hii yatufundisha jinsi inawapasa Wakristo kumwabudu Mungu. Katika mistari 21 Yesu alimwambia mwanamke, "saa inakuja ambayo hamtamwabudu Baba katika mlima huu wala kule Yerusalemu." Yesu anasema kwamba lazima ibada ya kweli kufanyika mahali fulani maalum ili Mungu apendezwe nayo. Siku hizi, wengine hufikiri kwamba Mungu aabudiwa katika jengo la kanisa, tu. Lakini, Yesu husema kwamba ibada ya kweli haitokani na mahali pale. Mistari 22 husema kwamba Wasamaria "Mnaabudu msichokijua. "Maana yake, inawezekana watu kuabudu kwa hali ya kutojua, wasipojua jinsi ya kuabudu katika kweli. Mistari 23 na 24 yafundisha neno muhimu zaidi. Waabudu halisi humwabudu Mungu katika roho na kweli. Lengo la ibada ni Mungu. Jinsi au nia ya ibada ni kirohoni, na matendo ya ibada ni matendo ya kweli, yaani kulingana na mapenzi yake Mungu.

Ibada ya Mtu Peke Yake

Kumwabudu Mungu si jambo linalofanyika na Wakristo pamoja wakati wa Jumapili. Paulo aandika katika *Warumi 12:1* kwamba inatupasa tutoe miili yetukama dhabihu iliyo hai na takatifu, ili kumpendeza Mungu. Kufanya hivyo ni huduma yetu ya ibada. Tunapaswa tutoe kabisa maisha yetu kwa ajili ya Mungu. Imetupasa maisha yetu yote kuwa matendo ya ibada na upendo kwa Mungu. Imetupasa maneno na matendo yetu yote kuwa matendo ya ibada na upendo kwa Mungu. Biblia inasema katika *Wagalatia 2:20* jinsi tunaweza kuishi hivi. Tulisulubishwa na Kristo. Na Kristo aishi ndani uetu kwa njia ya imani.

Mkutano wa Kristo

Akitarajia sisi kumwabudu peke yetu na kisiri, Mungu pia huamuru ibada ya mkutano wa watu. Mungu ataka Wakristo wote wakutane kila siku ya kwanza ya juma waabudu pamoja. Soma *Waebrania 10:25.* Mstari huo hutufudisha kwamba haitupasi tukose kuhudhuria kila mkutano wa kanisa.

Mungu ametuonyesha mapenzi yake kuhusu makutano wa ibada. Hatuacha bila kielelezo cha ibada inayompendeza. Tukifuata amri za Mungu katika ibada, tutafanya yafuatayo tunapokutana kwa ibada ya siku ya kwanza ya juma:

KUIMBA

Agano jipya likitaja muziki maana yake ni kuimba. "Wimbo" uliimbwa na Yesu na wanafunzi wake *Mathayo 26:30; Marko 14:26.* Paulo na Sila waliimba gerezani *Matendo 16:25.* Wakristo huambiwa waimbe kwa roho na akili *1 Wakorintho 14:15.*

Aina ya nyimbo zinaitwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni *Waefeso 5:19.* Imetupasa kumwimbia Mungu miyoni kulingana na *Wakolosai 3:16,17.* Kuimba ni "tunda la midomo" *Waebrania 13:15.* Wakristo wanapaswa kutangaza furaha yao kwa baraka za Mungu katika nyimbo *Yakobo 5:13.*

KUOMBA

Ziko amri nyingi na mifano mingi za maombi katika Agano Jipya. Katika *Mathayo 5:6-13,* Yesu afundisha mitume kusali. Katika 1 *Wathesalonike 5:17,* Wakristo waambiwa kuomba daima. Tunasoma kwamba wanaume wapaswa kuomba po pote katika 1 *Timotheo 2:8. Yakobo 5:13-16* hutuambia kuombeana. *1 Timotheo 2:1* husema, "kabla ya mambo yote nataka dua, sala, maombezi na shukrani zifanyike kwa ajili ya watu wote."

Mungu hupendezwa na maombi ya Wakristo wakati wo wote. Ni sehemu maalum katika ibada ya Kikristo kwa kuombea Baba. Kufanya hivi ni haki na tena njema.

KUHUBIRI na KUFUNDISHA

2 Timotheo 4:2 husema, "lihubiri neno." Tena, katika *Warumi 10:14-17* Paulo huuliza, "wamsikiaje pasipo mhubiri?" Kwa kuwa imani hutokana na kusikia neno la Mungu. Hakuna anayeweza kuamini pasipo kupokea neno. Kuhubiri na kufundishana ni mambo ya msingi kwa imani ya Kikristo.

Kuhubiri na kufundishana si kwa ajili ya wasioamini, tu. Katika *Waefeso 4:11-16,* Biblia yatufundisha kwamba mahubiri husaidia Wakristo wazidi katika imani ili waendeleze kazi ya kanisa. *Matendo 20:7* inahusu ibada ya Kikristo katika siku za Agano Jipya. Katika ibada hiyo, kuhubiri kulikuwa muhimu sana. Kanisa likutanapo siku hizi, tuhubiri na kufundisha kama vile walivyo fanya Wakristo wa zamani.

MEZA LA BWANA

Meza la Bwana lilianzishwa na Yesu mwenyewe alipokula na wanafunzi wake kabla hajakufa Mathayo *26:26-30; Marko 14:22-25; Luka 22:17-20.* Soma kwa uangalifu *1 Wakorintho 10:15-21 na 1 Wakorintho 11:17-20.* Maandiko haya yatwambia kuhusu umuhimu wa meza la Bwana. Kwanza, meza hilo ni wakati wa kukumbuka. Imetupasa kukumbuka kilo cha Yesu na mwili na damu yake tunapokula mkate na kunywa divai *1 Wakorintho 11:25-33.* Tusipokumbuka kifo cha Yesu tusiposhiriki meza la Bwana, tunayo hatia ya dhambi. Ya pili, meza la Bwana ni wakati wa kuonyesha imani yetu kwa wengine. Tunapokula mkate na kunywa divai, twaonyesha kwa matendo kwamba tunamwamini Yesu na kungojea kurudi kwake. Ni njia ya kuwaambia wengine kuhusu kifo cha Yesu kwa ajili ya dhambi za ulimwengu *1 Wakorintho 11:26.* Ya tatu, meza la Bwana ni wakati wa kuliangalia kindani. Wakristo wanaposhiriki meza la Bwana, imewapsa wajihoji ili wahakikishe

kwamba nia zao ni safi. Kila Mkristo ahakikishe kwamba anashiriki meza la Bwana kwa roho njema. Maana, afikirie kweli kifo cha Bwana na kukikumbuka, badala ya kula kunywa, tu *1 Wakorintho 11:28-37.* Sharti meza la Bwana lipokelewe kila siku ya kwanza ya juma Wakristo wakuatanapo pamoja. *Matendo 20:7* hutufundisha kwamba Wakristo wa siku za Agano Jipya walifuata kielelezo hicho. Twajua kwamba yaliyofundishwa katika kanisa moja yalifundishwa kwa makanisa yote wakati wa siku za mitume *1 Wakorintho 4:17*. Kwa hivyo, lazima kula meza la Bwana Jumapili ni kawaida ya makanisa yote. Tukiwa Wakristo wanaoamini Biblia siku hizi imetupasa tufanye vivyo hivyo.

SADAKA

Mtume Paulo aliandika kitabu cha Wafilipi alipokuwako gerezani na kuhitaji pesa. Wakristo wa rnji wa Filipi wakamtumia usaidizi. Paulo alisema kwamba kipawa chao kilikuwa kama harufu tamu, dhabihu iliyopendeza, na kumpendeza Mungu. Wakristo ni watoaii. Mkristo asiyetoa mali yake kwa ajili ya kazi ya Bwana ameanguka kutoka kwa upendo na imani. Biblia husema kwamba Wakristo waweke akiba kila siku ya kwanza ya jurna kwa ajili ya kazi ya Mungu. Ni sharti tufanye hivyo tunapokutana pamoja. Maandlko hutufundisha kutoa kwa njia hizi:

1. Kama kawaida 1 Wakorintho 16:1- 2
2. Kwa kusudia 1 Wakorintho 16:1,2; 2 Wakorintho 8:12-15
3. Watu wote watoe 1 Wakorintho 16:1-2
4. Kutoa Mengi 2 Wakorintho 8:1-4; 9:6-9
5. Kwa moyo wa mkujufu 2 Wakorintho 9:7
6. "Si kwa lazima 2 Wakorintho 8:12; 9:7

KENYA CHURCH OF CHRIST

TUNAWAKARIBISHA WOTE